# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# UCHAMBUZI WA UPIMAJI WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU (KKK) DARASA LA PILI 2018

**Imetolewa na:**
**Baraza la Mitihani la Tanzania**
**S. L. P. 2624**
**Dar es Salaam**

**JUNI, 2019**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# UCHAMBUZI WA UPIMAJI WA STADI ZA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU (KKK) DARASA LA PILI 2018

Kimetolewa na

Baraza la Mitihani la Tanzania
S.L.P. 2624
DAR ES SALAAM

**JUNI, 2019**

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019**

Haki zote zimehifadhiwa

YALIYOMO


Orodha ya Majedwali ........ VI

Orodha ya Chati ........ VII

Orodha ya Vielelezo ........ VIII

DIBAJI ........ X

SURA YA KWANZA ........ 1

SAMPULI, ZANA ZA UPIMAJI NA UCHAMBUZI WA TAKWIMU ........ 1

1.1 utangulizi ........ 1
1.2 Sampuli ya Upimaji ........ 1
1.3 Zana Zilizotumika Kufanya Upimaji ........ 1
1.4 Uchambuzi wa Takwimu za Upimaji wa Stadi za KKK 2018 ........ 2

SURA YA PILI ........ 3

UPIMAJI WA STADI YA KUSOMA ........ 3

2.1 Utangulizi ........ 3
2.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kusoma ........ 3
2.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi ya Kusoma ........ 3
2.4 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi ........ 4
2.4.1 Swali la 1: Umahiri wa Kusoma Maneno ........ 4
2.4.1.1 Utendaji wa Wanafunzi Wanaojifunza kwa Lugha ya Kiswahili ........ 7
2.4.1.2 Utendaji wa Wanafunzi Wanaojifunza kwa Lugha ya Kiingereza ........ 9
2.4.2 Swali la 2: Umahiri wa Kusoma Sentensi ........ 10
2.4.2.1 Utendaji wa Kusoma Sentensi kwa Wanafunzi Wanaojifunza kwa Lugha ya Kiswahili ........ 14
2.4.2.2 Utendaji wa Kusoma sentensi kwa Wanafunzi Wanaojifunza kwa Lugha ya Kiingereza ........ 15
2.4.3 Swali la 3: Umahiri wa Kujenga Ufahamu Katika Kusoma ........ 17
2.4.4 Ulinganifu wa utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Sentensi na Kifungu cha Maneno ........ 21
2.4.5 Utendaji wa Wanafunzi Katika Kujenga Ufahamu wa Kusoma Kifungu cha maneno kwa Wanafunzi Wanaotumia Lugha ya Kiswahili Kujifunzia ........ 21
2.4.6 Utendaji wa Wanafunzi katika Kujenga Ufahamu wa Kusoma Kifungu cha Maneno kwa Wanafunzi wanaojifunza kwa Lugha ya Kiingereza ........ 23
2.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia, Mahali Shule ilipo, Jinsi na shule Zilizopimwa Mwaka 2017 na kurudia Kupimwa Mwaka 2018 ........ 25
2.5.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Stadi ya Kusoma kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia ........ 25
2.5.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Mahali Shule Ilipo ........ 26

2.5.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi……………………..27
2.5.4 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Shule 66 Zilizopimwa Mwaka 2017 na Mwaka 2018........................................................................................ 28
2.5.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Shule 33 zilizopimwa mwaka 2017 na kupimwa tena 2018 ........................................................................................ 29
2.6 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi ya Kusoma........................................30

SURA YA TATU........................................................................................ 31

UPIMAJI WA STADI YA KUANDIKA........................................................................ 31

3.1 Utangulizi........................................................................................31
3.2 Muundo wa karatasi ya upimaji wa stadi ya kuandika..................................31
3.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi ya Kuandika kwa kila Umahiri ........................31
3.4 Uchambuzi wa Takwimu za Majibu ya Wanafunzi........................................32

3.4.1 Utendaji wa Wanafunzi Katika Kutambua Picha na Kuandika Jina la Picha Husika.. 32

3.4.2 Umahiri wa Wanafunzi katika Kutambua Herufi Kubwa........................................ 40

3.4.3 Umahiri wa Kunakili Kifungu cha Maneno na Kuweka Alama za Uandishi ................. 42

3.5 Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia lugha ya kufundishia, mahali shule ilipo utendaji wa wanafunzi mwaka 2017 na 2018, shule 33 zilizofanya upimaji mwaka 2017 na kurudia 2018 ........................................................................46
3.5.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia.............46
3.5.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Shule za Mijini na Vijijini.......................47
3.5.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Waliofanya Upimaji mwaka 2017 Ikilinganishwa na Mwaka 2018 ....................................................................49
3.5.4 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Shule 33 Zilizopimwa mwaka 2017 na Kupimwa kwa mara nyingine 2018 ..................................................................50
Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi wa shule 33 zilizopimwa mwaka 2017 na kufanya upimaji kwa mara ya pili mwaka 2018 umefanyika. Matokeo ya ulinganifu wa utendaji wao yameoneshwa katika Chati Na. 18. ......................................................50
3.5.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Jinsi................................................50
3.6 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi ya Kuandika............................................51

SURA YA NNE........................................................................................ 52

UPIMAJI WA STADI YA KUHESABU ........................................................................ 52

4.1 Utangulizi........................................................................................52
4.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kuhesabu......................................52
4.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi ya Kuhesabu..................................................52
4.4 Utendaji wa Jumla Katika Stadi ya Kuhesabu....................................................52
4.5 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi ...............................................................53
4.5.1 Umahiri wa Kutambua Namba Inayokosekana katika Mpangilio wa Namba ...............53
4.5.2 Umahiri wa Kujumlisha ...............................................................................56

4.5.3 Umahiri wa Kutoa ... 59
4.5.4 Umahiri wa Kufumbua Mafumbo ... 62
4.6 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia, Mahali Shule ilipo, Jinsi na Shule Zilizofanya Upimaji Mwaka 2017 na 2018 na Shule 33 Zilizopimwa Mwaka 2017 na 2018 ... 68
4.6.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia ... 68
4.6.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Shule za Mijini na Vijijini ... 69
4.6.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi ... 70
4.6.4 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Shule 33 Zilizopimwa Mwaka 2017 na Kupimwa Tena 2018 ... 70
4.6.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Shule 33 Zilizopimwa kwa Mara ya Kwanza na Mara Pili Mwaka 2018 ... 71
4.6.6 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi mwaka 2017 na 2018 ... 72
4.6 Muhtasari wa uchambuzi katika stadi ya kuhesabu ... 73

SURA YA TANO ... **74**

UCHAMBUZI WA TAARIFA ZA USIMAMIZI ... **74**

5.1 Uchambuzi wa taarifa za shule ... 74

5.1.1 Taarifa za shule kwa ujumla ... **74**

5.1.2 Ufundishaji wa wanafunzi na mafunzo kwa walimu wa stadi za KKK ... **76**

5.1.3 Hali ya vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia ... **76**

5.1.4 Miundombinu na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ... **77**

5.1.5 Mahudhurio ya wanafunzi ... **78**

SURA YA SITA ... **80**

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ... **80**

6.1 Hitimisho ... 80
6.2 Mapendekezo ... 81

Kiambatisho na. 1: Karatasi ya upimaji stadi ya kusoma ... **82**

Kiambatisho na. 3: Reading skills ... **92**

Kiambatisho na. 4: Reading assesssment scale ... **98**

Kiambatisho na. 5: Karatasi ya upimaji stadi ya kuandika ... **103**

Kiambatisho na. 6: Writing skills ... **107**

Kiambatisho na. 7: Karatasi ya upimaji stadi ya kuhesabu ... **111**

Kiambatisho na. 8: Arithmetic skills ... **115**

Kiambatisho na. 9: Dodoso la mwalimu mkuu ... **119**

Kiambatisho na. 10: Dodoso la msimamizi ........................................................................................123

## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Utendaji wa Wanafunzi Mwaka 2017 na 2018 .......... 2
Jedwali Na. 2: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Maneno .......... 4
Jedwali Na. 3: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Maneno ya Kiswahili .......... 7
Jedwali Na. 4: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Maneno ya Kiingereza .......... 9
Jedwali Na. 5: Utendaji wa Wanafunzi katika Kujibu Maswali ya Ufahamu .......... 18
Jedwali Na. 6: Utendaji wa Wanafunzi katika Umahiri wa Kusoma kwa Ufahamu .......... 22
Jedwali Na. 7: Asilimia ya Wanafunzi walioshindwa Kujibu Swali la Ufahamu kwa kila Kipengele .......... 23
Jedwali Na. 8: Utendaji wa Wanafunzi katika Kujibu Swali la Ufahamu .......... 24
Jedwali Na. 9: Utendaji wa Jumla wa Stadi ya Kuandika .......... 32
Jedwali Na. 10: Umahiri wa Wanafunzi wa Kunakili na Kutumia Alama za Uandishi .......... 43
Jedwali Na. 11: Ulinganifu wa Utendaji kwa Shule za Mijini na Vijijini .......... 48
Jedwali Na. 12: Ulinganifu wa Utendaji wa wanafunzi waliofanya Upimaji mwaka 2017 na 2018. .......... 49
Jedwali Na. 13: Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Jinsi .......... 51
Jedwali Na. 14: Utendaji wa Jumla katika Stadi ya Kuhesabu .......... 53
Jedwali Na. 15: Idadi ya Wanafunzi katika Mkondo .......... 75
Jedwali Na. 16: Upatikanaji wa Vitabu na Vifaa vya Kujifunzia KKK .......... 76
Jedwali Na. 17: Muhtasari wa Majibu ya Walimu Kuhusu Mazingira ya Kujifunzia KKK .......... 78
Jedwali Na. 18: Taarifa za Wanafunzi Wasiofanya Upimaji .......... 79

## Orodha ya Chati


Chati Na. 1: Asilimia ya Wanafunzi Walioweza Kusoma Kila Neno .................................... 8
Chati Na. 2: Asilimia ya Wanafunzi Walioshindwa Kusoma Maneno ya Kiingereza.......... 10
Chati Na. 3: Utendaji wa Wanafunzi Katika Kusoma Sentensi. ....................................... 11
Chati Na. 4: Utendaji wa Wanafunzi Katika Usomaji wa Sentensi za Kiswahili. ................ 15
Chati Na. 5: Utendaji wa Wanafunzi Katika Usomaji wa Sentensi za Kiingereza. ............. 16
Chati Na. 6: Utendaji wa Wanafunzi kwa Kila Kipengele cha Swali. ................................ 21
Chati Na. 7: Asilimia ya Utendaji wa Wanafunzi Katika kila Kipengele ............................ 23
Chati Na. 8: Asilimia ya Utendaji wa Wanafunzi Katika kila Kipengele ............................ 25
Chati Na. 9: Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Wanaotumia Lugha ya Kiingereza na Kiswahili. ......................................................................................................... 26
Chati Na. 10: Utendaji wa Wanafunzi Wanaosoma Shule za Mjini na Wanaosoma Shule za Vijijini. ......................................................................................................... 27
Chati Na. 11: Ulinganifu wa Utendaji kati ya Wavulana na Wasichana. ............................ 28
Chati Na. 12: Ulinganifu wa Shule Zilizopimwa Mwaka 2017 na 2018 ............................. 29
Chati Na. 13: Ulinganifu wa Shule 33 Zilizopimwa Mwaka 2017 na Kupimwa tena 2018. . 29
Chati Na. 14: Utendaji wa Wanafunzi katika Kuandika Majina ya Picha. .......................... 33
Chati Na. 15: Utendaji wa wanafunzi katika kutambua herufi kubwa ............................... 41
Chati Na. 16: Utendaji wa wanafunzi katika Stadi ya Kuandika kwa shule zinazotumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza. ........................................................... 47
Chati Na. 17: Ulinganifu wa Utendaji wa wanafunzi kutoka shule za Mjini na Vijijini. ........ 48
Chati Na. 18: Matokeo ya ulinganifu wa shule 33 zilizopimwa mwaka 2017 na 2018...... 50
Chati Na. 19: Asilimia ya Wanafunzi waliojibu swali la 1 hadi 5 kwa usahihi .................... 54
Chati Na. 20: Wanafunzi Waliojibu Swali la 6 hadi 10 kwa Usahihi. ................................ 57
Chati Na. 21: Asilimia ya wanafunzi waliojibu swali la 11 hadi 15 kwa usahihi. ................ 60
Chati Na. 22: Asilimia ya wanafunzi waliojibu swali la 16 hadi 20 kwa usahihi. ................ 62
Chati Na. 23: Ulinganifu wa Utendaji kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia. .................... 68
Chati Na. 24: Ulinganifu wa Utendaji kwa Shule za Mijini na Vijijini ................................. 69
Chati Na. 25: Ulinganifu wa Utendaji kwa kuzingatia jinsi. ............................................... 70
Chati Na. 26: Ulinganifu wa Utendaji kwa Shule zilizopimwa 2017 na kupimwa kwa mara nyingine mwaka 2018. ......................................................................... 71
Chati Na. 27: Ulinganifu wa Utendaji kwa Shule zilizopimwa kwa mara ya kwanza na shule zilizopimwa mara ya pili. ...................................................................... 71
Chati Na. 28: Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa Shule 66 zilizofanya upimaji 2017 na 2018.......................................................................................... 72

## Orodha ya Vielelezo


Kielelezo Na 1: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno ishirini na tano (25) kwa ufasaha. .... 5
Kielelezo Na 2: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno kumi na nne (14). .... 5
Kielelezo Na 3: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno manane (8). .... 6
Kielelezo Na 4: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma neno moja hadi maneno sita .. 6
Kielelezo Na 5: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kusoma maneno yote. .... 7
Kielelezo Na 6: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno ishirini na tano (25). 11
Kielelezo Na 7: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno 16. .... 12
Kielelezo Na 8: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno 7 hadi 13. .... 12
Kielelezo Na 9: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma neno 1 hadi maneno 6 .... 13
Kielelezo Na 10: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kusoma maneno yote katika sentensi walizopewa. .... 13
Kielelezo Na 11: Sampuli ya majibu ya wanafunzi waliojibu vipengele vinne kwa usahihi .... 18
Kielelezo Na 12: Majibu ya wanafunzi waliojibu vipengele vitatu vya swali kwa usahihi. .... 19
Kielelezo Na 13: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kujibu vipengele viwili vya swali kati ya vinne kwa usahihi na kupata alama za wastani. .... 19
Kielelezo Na 14: Majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu vipengele vyote vya swali hili. .... 20
Kielelezo Na 15: Majibu ya wanafunzi walioweza kuandika majina ya picha kwa usahihi. .... 34
Kielelezo Na 16: Majibu ya wanafunzi walioshindwa kuandika majina ya picha kwa usahihi. .... 35
Kielelezo Na 17: Majibu ya Wanafunzi waliopigia mistari kwa usahihi maneno yote yaliyoundwa kwa herufi kubwa. .... 41
Kielelezo Na 18: Majibu ya Wanafunzi waliopigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo au kupigia mstari maneno yote. .... 42
Kielelezo Na 19: Majibu ya Wanafunzi ambao hawakupigia mstari neno lolote. .... 42
Kielelezo Na 20: Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi kwa usahihi. .... 43
Kielelezo Na 21: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweka alama za uandishi katika kifungu cha maneno na kunakili majina ya alama za uandishi. .... 44
Kielelezo Na 22: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyetunga maelezo binafsi yasiyo na uhusiano na kifungu cha maneno. .... 45
Kielelezo Na 23: Sampuli ya majibu ya wanafunzi waliotumia alama za uandishi mahali pasipokuwa sahihi katika kifungu cha maneno. .... 46
Kielelezo Na 24: Majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali la 3 na 5. .... 54
Kielelezo Na 25: Wanafunzi waliokosa umahiri katika kujaza namba zinazokosekana kwenye mfuatano wa namba. .... 55
Kielelezo Na 26: Majibu ya wanafunzi waliojaza kwa usahihi namba zinazokosekana katika swali la 1 hadi 5. .... 56
Kielelezo Na 27: Majibu ya wanafunzi waliojumlisha namba walizopewa kwa usahihi katika swali la 6 hadi 10. .... 57
Kielelezo Na 28: Mwanafunzi aliyeshidwa kujibu kwa usahihi swali la 8, 9 na 10. .... 58
Kielelezo Na 29: Majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali la 6 hadi 10 hivyo kuonekana kukosa umahiri katika dhana zilizopimwa. .... 59
Kielelezo Na 30: Majibu ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi swali la 11 na 12 na kushindwa swali la 13, 14 na 15. .... 60
Kielelezo Na 31: Majibu ya wanafunzi walioshindwa maswali yote yaliyopima dhana ya kutoa. .... 61

Kielelezo Na 32: Majibu ya wanafunzi waliojibu swali la 11 hadi 15 kwa usahihi na hivyo kuonekana kuwa na umahiri wa kujumlisha ngazi ya kwanza na ya pili. .................................. 62
Kielelezo Na 33: Majibu ya mwanafunzi aliyejibu swali la 16 hadi 20 kwa usahihi. .......................... 64
Kielelezo Na 34: Mwanafunzi aliyetumia matendo ya kutoa na kujumlisha kimakosa katika swali la 16, 17 na 19. Katika swali la 18 na 20 alitumia matendo sahihi lakini alikosea katika kujumlisha au kutoa namba zilizotolewa...................................................... 67
Kielelezo Na 35: Sampuli ya majibu mwanafunzi yasiyoeleweka...................................................... 67

## DIBAJI

Upimaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa wanafunzi wa Darasa la Pili mwaka 2018 ulifanywa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa lengo la kubaini umahiri wa wanafunzi katika kumudu stadi hizo. Jumla ya shule za msingi 66 kutoka wilaya 22 za mikoa 11 inayowakilisha kanda za kielimu Tanzania Bara ziliteuliwa kufanya Upimaji. Shule 3 ziliteuliwa katika kila Halmashauri kwa kuzingatia mazingira ya kijijini na mjini ambapo shule mbili zilikuwa zinatumia lugha ya Kiswahili na moja inatumia lugha ya Kiingereza kujifunzia na kufundishia. Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania liliandaa zana za upimaji kwa Stadi zote tatu na dodoso kwa ajili ya Mwalimu Mkuu na Wasimamizi walioteuliwa kusimamia Upimaji.

Wanafunzi 6,941 walisajiliwa kufanya upimaji wa Stadi za KKK. Kati yao, 5,621 sawa na asilimia 80.98 walifanya upimaji. Aidha, wanafunzi 1,320 sawa na asilimia 19.02 hawakufanya upimaji huo kutokana na sababu mbalimbali.

Usahihishaji na uchambuzi wa majibu ya wanafunzi ulifanywa ili kubaini viwango vya utendaji wa wanafunzi katika kila Stadi. Uchambuzi wa viwango vya kufaulu unaonesha kuwa, utendaji wa wanafunzi waliofanya upimaji ulikuwa mzuri katika stadi zote tatu. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi wengi (90.22%) walikuwa na utendaji mzuri katika Stadi ya Kusoma ikilinganishwa na Stadi ya Kuandika (89.18%) na Kuhesabu (77.49%).

Taarifa ya uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi imeainishwa katika sura sita. Sura ya Kwanza ni Utangulizi na Sura ya Pili hadi ya Nne inahusu Upimaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu mtawalia. Sura ya Tano inaelezea Uchambuzi wa Taarifa za Usimamizi na Sura ya Sita ni Maoni, Mapendekezo na Hitimisho.

Baraza la Mitihani linaamini kuwa taarifa hii itakuwa ni mrejesho na kichocheo kwa wadau wa Elimu kwa lengo la kuimarisha ufundishaji wa Stadi za KKK na hivyo kuimarisha umahiri wa wanafunzi katika kumudu Stadi hizo.

Dkt. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

# SURA YA KWANZA

## SAMPULI, ZANA ZA UPIMAJI NA UCHAMBUZI WA TAKWIMU

### 1.1 Utangulizi

Baraza la Mitihani la Tanzania lilifanya upimaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kwa wanafunzi wa Darasa la Pili. Upimaji huo ulihusisha wanafunzi wa darasa la tatu kwa mwaka 2019 waliomaliza mtaala wa darasa la kwanza na la pili mwaka 2018. Upimaji ulifanyika tarehe 11/04/2019 na tarehe 12/04/2019 na ulilenga kupima umahiri wa wanafunzi katika stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Katika Stadi ya Kusoma wanafunzi walipimwa umahiri wa kutambua sauti, herufi na kujenga ufahamu katika kusoma na kusikiliza. Katika Stadi ya Kuandika wanafunzi walipimwa umahiri wa uundaji wa maneno, kubainisha uumbaji wa herufi kubwa na ndogo na kunakili kifungu cha maneno na kutumia alama za uandishi. Aidha, katika Stadi ya Kuhesabu, wanafunzi walipimwa umahiri wa kutambua namba inayokosekana katika mpangilio wa namba, kujumlisha na kutoa namba isiyozidi 999 na kufumbua mafumbo.

### 1.2 Sampuli ya Upimaji

Upimaji ulifanyika katika shule 66 zilizoteuliwa kutoka wilaya mbili za mikoa 11 ambayo ni Arusha, Dar es Salaam, Kagera, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Njombe, Singida na Tabora. Aidha, shule tatu ziliteuliwa kwa kila wilaya ambapo shule mbili zilikuwa zinatumia mfumo wa lugha ya Kiswahili na moja lugha ya Kiingereza katika kujifunzia na kufundishia.

Wanafunzi 6,941 walisajiliwa kufanya upimaji katika stadi zote. Kati yao, 5,621 walifanya upimaji wa Stadi ya Kusoma, 5,677 Stadi ya Kuandika na 5,682 Stadi ya Kuhesabu. Mahudhurio ya wanafunzi katika upimaji huu yalitofautiana kati ya stadi moja na nyingine kutokana na sababu za ama utoro, ugonjwa au uhamisho.

### 1.3 Zana Zilizotumika Kufanya Upimaji

Zana zilizotumika katika upimaji ni karatasi za maswali ya Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (Kiambatisho.Na.1 hadi 8). Maswali yaliyotungwa kwa kila stadi yalilenga kupima umahiri wa wanafunzi kwa kuzingatia viwango vya utendaji. Aidha, madodoso yaliandaliwa kwa ajili ya wasimamizi na walimu wakuu ili kupata taarifa kuhusu walimu wanaofundisha stadi za KKK, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na hali ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa jumla (Kiambatisho Na. 9 na 10).

## 1.4 Uchambuzi wa Takwimu za Upimaji wa Stadi za KKK 2018

Uchambuzi wa takwimu katika stadi ya Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ulifanyika kwa lengo la kubaini umahiri wa wanafunzi katika utendaji wao kwa kila stadi. Umahiri huo ulipimwa kwa kuzingatia vigezo vya utendaji ambapo utendaji ulikuwa hafifu ikiwa mwanafunzi alipata alama 0 – 12, wastani 13 – 25, mzuri 26 – 38 na mzuri sana 39 – 50. Aidha, ulinganifu wa utendaji wa mwaka 2017 na 2018 umefanyika. Uchambuzi wa viwango vya utendaji umewasilishwa kwa kutumia Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1: Utendaji wa Wanafunzi Mwaka 2017 na 2018**

| Stadi | Waliofanya | | Wanafunzi waliokuwa na Utendaji wa Wastani hadi Mzuri sana | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017 | 2018 | 2017 | | 2018 | | Ongezeko (%) |
| | | | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | |
| Kusoma | 6,464 | 5,621 | 5,681 | 90.13 | 5,071 | 90.22 | 0.09 |
| Kuandika | 6,174 | 5,677 | 5,486 | 88.86 | 5,063 | 89.18 | 0.32 |
| Kuhesabu | 6,195 | 5,682 | 4,767 | 76.95 | 4,403 | 77.49 | 0.54 |

Wakati wa uchambuzi, sampuli za majibu ya wanafunzi zimetumika ili kuonesha umahiri wa wanafunzi katika utendaji wao na changamoto walizokuwa nazo katika stadi husika. Uchambuzi wa takwimu ulihusisha pia ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi waliofanya upimaji mwaka 2017 na 2018.

Kwa ujumla, utendaji wa wanafunzi kwa mwaka 2018 ulikuwa mzuri ikilinganishwa na mwaka 2017 ambapo viwango vya utendaji vimeongezeka katika stadi zote. Utendaji wa wanafunzi katika Stadi ya Kusoma umeongezeka kwa asilimia 0.09 wakati utendaji wa Kuandika una ongezeko la asilimia 0.33 na Stadi ya Kuhesabu umeongezeka kwa asilimia 0.54.

# SURA YA PILI

## UPIMAJI WA STADI YA KUSOMA

### 2.1 Utangulizi

Uchambuzi wa Stadi ya Kusoma umefanyika ili kubaini uwezo wa wanafunzi katika kusoma maneno, sentensi na kifungu cha maneno kwa lengo la kupima uelewa wa jambo walilosoma. Uchambuzi umezingatia vigezo vya utendaji wa wanafunzi katika usomaji wa maneno, sentensi na kifungu cha maneno. Umahiri wa wanafunzi katika swali la kwanza ulitegemea idadi ya maneno ambayo wanafunzi wameweza kusoma kwa ufasaha ndani ya dakika moja. Katika swali la pili umahiri wa wanafunzi ulipimwa kwa kuzingatia uwezo wa wanafunzi kusoma maneno katika sentensi kwa mtiririko unaoleta mantiki. Aidha, katika swali la tatu umahiri wa wanafunzi ulitegemea uwezo wa wanafunzi kujibu maswali yaliyotokana na kifungu cha maneno walichokisoma. Kwa ujumla, ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi ulifanyika kwa kuzingatia lugha ya kujifunzia, mahali shule ilipo (mjini/vijijini), jinsi na shule zilizofanya upimaji mwaka 2017 na 2018.

### 2.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kusoma

Karatasi ya upimaji wa Stadi ya Kusoma iliandaliwa kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza kutegemea lugha inayotumiwa na shule husika kufundishia na kujifunzia. Jumla ya maswali matatu yaliandaliwa ambapo swali la kwanza lilipima umahiri wa mwanafunzi kusoma maneno ishirini na tano (25), la pili lilipima umahiri wa mwanafunzi kusoma sentensi kwa mtiririko unaoleta mantiki na swali la tatu lilipima umahiri wa mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno na kujibu maswali kwa mdomo.

Mwanafunzi alitumia dakika tano (5); kusoma maneno, sentensi na kifungu cha maneno kisha kujibu maswali kwa mdomo. Msimamizi alitumia dakika kumi (10) kwa ajili ya kujaza alama za mwanafunzi wakati anasoma, kukokotoa na kujaza alama za mwanafunzi katika skeli ya upimaji kwa maswali yote. Hivyo upimaji ulitumia dakika 15 kwa kila mwanafunzi.

### 2.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi ya Kusoma

Utendaji wa mwanafunzi katika Stadi ya Kusoma uligawanyika katika makundi manne. Mwanafunzi alikuwa na utendaji mzuri sana kwa kuweza kusoma maneno 20-25 kwa usahihi ndani ya dakika moja, 14-19 utendaji mzuri, 7 -13 wastani na 0- 6 hafifu katika swali la kwanza na la pili.

Utendaji wa umahiri wa mwanafunzi katika kusoma kifungu cha habari na

kujibu maswali kwa mdomo ulipimwa kwa kuzingatia idadi ya vipengele alivyoweza kujibu ndani ya dakika tatu. Mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi vipengele vinne alikuwa na utendaji mzuri sana, vitatu utendaji mzuri, viwili utendaji wa wastani na aliyejibu kipengele kimoja au kushindwa vyote utendaji hafifu.

## 2.4 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi

Jumla ya wanafunzi 6,941 walisajiliwa kufanya upimaji wa Stadi ya Kusoma. Kati yao wanafunzi 5,621 sawa na asilimia 80.98 walifanya upimaji huo. Wavulana walikuwa 2,777 na wasichana 2,844. Idadi ya wanafunzi waliofanya upimaji kwa lugha ya Kiswahili ni 4,698 na kwa lugha ya Kiingereza ni 923. Matokeo ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Stadi ya Kusoma yanaonesha kuwa, asilimia 90.22 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Utendaji wa wasichana ni asilimia 91.87 na wavulana asilimia 88.44 ambapo wasichana wamekuwa na utendaji wa juu zaidi kwa asilimia 3.43.

### 2.4.1 Swali la 1: Umahiri wa Kusoma Maneno

Swali lilipima umahiri wa mwanafunzi kusoma maneno ishirini na tano kwa ufasaha kwa muda wa dakika moja. Utendaji wa wanafunzi katika kusoma maneno ulikuwa wa wastani hadi mzuri sana kwani asilimia 89.91 ya wanafunzi waliweza kusoma maneno 7 hadi 25 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2

**Jedwali Na. 2: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Maneno**

| Maneno | Utendaji | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 0 – 6 | Hafifu | 567 | 10.09 |
| 7 – 13 | Wastani | 238 | 4.23 |
| 14 – 19 | Mzuri | 414 | 7.37 |
| 20 – 25 | Mzuri Sana | 4,402 | 78.31 |
| **Jumla** | | **5,621** | **100.00** |

Jedwali Na. 2 linaonesha kuwa, jumla ya wanafunzi 4,402 sawa na asilimia 78.31 walikuwa na utendaji mzuri sana kwani waliweza kusoma kwa ufasaha maneno 20 hadi 25. Idadi ya maneno hayo ni zaidi ya robo tatu ya maneno yote waliyotakiwa kusoma katika swali hili. Kielelezo Na. 1 ni sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno yote kwa usahihi.

1. Kusoma maneno (alama 12$^1/_2$)

Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi alipokosea kusoma neno na akarudia kwa usahihi, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama 00$^1/_2$**)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| televisheni | gita | vitamini | Wiki | Picha |
| kompyuta | pini | mdomo | sentensi | nyumba |
| tochi | baiskeli | mwanafunzi | ubao | mwavuli |
| chumvi | saa | mbwa | mwezi | kikombe |
| mchele | mkono | mwanga | karoti | jogoo |

1. Reading of words (12$^1/_2$ marks)

Put a **slanted slash mark (/)** in each word which the pupil has **failed** to read. Circle **(Ø)** if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed. (The score for each correct word is **00$^1/_2$ mark**)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| television | guitar | vitamins | week | picture |
| computer | pin | mouth | sentence | house |
| torch | bicycle | pupil | blackboard | umbrella |
| salt | watch | dog | moon | cup |
| rice | arm | light | carrot | cock |

**Kielelezo Na 1:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno ishirini na tano (25) kwa ufasaha.

Wanafunzi 414 sawa na asilimia 7.37 walikuwa na utendaji mzuri kwa kuweza kusoma kwa ufasaha maneno 14 hadi 19 ambayo ni zaidi ya nusu ya maneno yote. Kielelezo Na. 2 ni sampuli ya majibu ya wanafunzi waliopata utendaji mzuri.

1. Kusoma maneno (alama 12$^1/_2$)

Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi alipokosea kusoma neno na akarudia kwa usahihi, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama 00$^1/_2$**)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| televisheni | ~~gita~~ | vitamini | Wiki | Picha |
| ~~kompyuta~~ | pini | ~~mdomo~~ | ~~sentensi~~ | nyumba |
| tochi | baiskeli | mwanafunzi | ubao | mwavuli |
| ~~chumvi~~ | saa | mbwa | mwezi | ~~kikombe~~ |
| ~~mchele~~ | ~~mkono~~ | ~~mwanga~~ | ~~karoti~~ | ~~jogoo~~ |


1. Reading of words (12$^1/_2$ marks)

Put a **slanted slash mark (/)** in each word which the pupil has **failed** to read. Circle **(Ø)** if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed. (The score for each correct word is **00$^1/_2$ mark**)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ~~television~~ | ~~guitar~~ | vitamins | week | ~~picture~~ |
| ~~computer~~ | pin | mouth | sentence | house |
| ~~torch~~ | ~~bicycle~~ | pupil | ~~blackboard~~ | ~~umbrella~~ |
| salt | watch | dog | moon | cup |
| ~~rice~~ | arm | ~~light~~ | carrot | ~~cock~~ |

**Kielelezo Na 2:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno kumi na nne (14).

Aidha, wanafunzi 238 sawa na asilimia 4.23 waliweza kusoma kwa ufasaha maneno 7 hadi 13. Wanafunzi hao walikuwa na utendaji wa wastani kwa sababu waliweza kusoma maneno ambayo ni chini ya nusu au nusu ya maneno yote. Kielelezo Na. 3 ni sampuli ya majibu ya wanafunzi waliokuwa na utendaji wa wastani.



1. Kusoma maneno (alama $12^1/_2$)

Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi alipokosea kusoma neno na akarudia kwa usahihi, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama $00^1/_2$**)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| televisheni | gita | vitamini | Wiki | Picha |
| kompyuta | pini | mdomo | sentensi | nyumba |
| tochi | baiskeli | mwanafunzi | ubao | mwavuli |
| chumvi | saa | mbwa | mwezi | kikombe |
| mchele | mkono | mwanga | karoti | jogoo |


1. Reading of words ($12^1/_2$ marks)

Put a **slanted slash mark (/)** in each word which the pupil has **failed** to read. Circle **(Ø)** if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed. (The score for each correct word is **$00^1/_2$ mark**)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| television | guitar | vitamins | week | picture |
| computer | pin | mouth | sentence | house |
| torch | bicycle | pupil | blackboard | umbrella |
| salt | watch | dog | moon | cup |
| rice | arm | light | carrot | cock |

**Kielelezo Na 3:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno manane (8).

Hata hivyo, wanafunzi 567 sawa na asilimia 10.09 walikuwa na utendaji hafifu ambapo asilimia 4.86 waliweza kusoma kati ya neno 1 hadi maneno 6. Vile vile asilimia 5.23 hawakuweza kusoma maneno yote kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 4 na 5.



1. Kusoma maneno (alama $12^1/_2$)

Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi alipokosea kusoma neno na akarudia kwa usahihi, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama $00^1/_2$**)


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| televisheni | gita | vitamini | Wiki | Picha |
| kompyuta | pini | mdomo | sentensi | nyumba |
| tochi | baiskeli | mwanafunzi | ubao | mwavuli |
| chumvi | saa | mbwa | mwezi | kikombe |
| mchele | mkono | mwanga | karoti | jogoo |

1. Kusoma maneno (alama $12^1/_2$)

Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi alipokosea kusoma neno na akarudia kwa usahihi, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama $00^1/_2$**)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| televisheni | gita | vitamini | Wiki | Picha |
| kompyuta | pini | mdomo | sentensi | nyumba |
| tochi | baiskeli | mwanafunzi | ubao | mwavuli |
| chumvi | saa | mbwa | mwezi | kikombe |
| mchele | mkono | mwanga | karoti | jogoo |

**Kielelezo Na 4:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma neno moja hadi maneno sita



1. Kusoma maneno (alama 12¹/₂)

Weka alama ya **mkwaju** (/) kwa kila neno ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi alipokosea kusoma neno na akarudia kwa usahihi, zungushia (Ø) neno hilo. (Kila neno moja sahihi **alama 00¹/₂**)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| televisheni | gita | vitamini | Wiki | Picha |
| kompyuta | pini | mdomo | sentensi | nyumba |
| tochi | baiskeli | mwanafunzi | ubao | mwavuli |
| chumvi | saa | mbwa | mwezi | kikombe |
| mchele | mkono | mwanga | karoti | jogoo |

1. Reading of words (12¹/₂ marks)

Put a **slanted slash mark** (/) in each word which the pupil has **failed** to read. Circle (Ø) if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed. (The score for each correct word is **00¹/₂ mark**)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| television | guitar | vitamins | week | picture |
| computer | pin | mouth | sentence | house |
| torch | bicycle | pupil | blackboard | umbrella |
| salt | watch | dog | moon | cup |
| rice | arm | light | carrot | cock |

**Kielelezo Na 5:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kusoma maneno yote.

### 2.4.1.1 Utendaji wa Wanafunzi Wanaojifunza kwa Lugha ya Kiswahili


Wanafunzi wanaojifunza kwa lugha ya Kiswahili wameonesha kuwa na umahiri wa wastani hadi mzuri sana kwa asilimia 88.21. Wanafunzi hao waliweza kusoma maneno 7 hadi 25 kwa ufasaha. Aidha, asilimia 11.79 walikuwa na utendaji hafifu, kati yao asilimia 5.62 waliweza kusoma neno 1 hadi maneno 6 kwa usahihi. Hata hivyo, asilimia 6.17 walishindwa kusoma maneno yote kama inavyoonekana katika Jedwali Na.3.

**Jedwali Na. 3: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Maneno ya Kiswahili**

| Maneno | Utendaji | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 0 – 6 | Hafifu | 554 | 11.79 |
| 7 – 13 | Wastani | 212 | 4.51 |
| 14 – 19 | Mzuri | 342 | 7.28 |
| 20 – 25 | Mzuri Sana | 3,590 | 76.42 |
| **Jumla** | | **4,698** | **100.00** |

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi wengi waliweza kusoma kwa usahihi maneno ambayo yameundwa kwa silabi zenye

muundo wa konsonanti na irabu, kwa mfano, neno pini (89.17%). Aidha, utendaji wa wanafunzi katika kusoma maneno yenye silabi zenye muundo wa irabu pekee ulikuwa mzuri sana kwa sababu wakati wa kutamka irabu hewa hutoka bila kuzuiwa. Mfano wa maneno hayo ni saa (89.97%) na ubao (88.42%). Chati Na. 1 inaonesha utendaji wa wanafunzi kwa kila neno.




**Chati Na. 1:** *Asilimia ya Wanafunzi Walioweza Kusoma Kila Neno.*

Takwimu zaidi zinaonesha kuwa, yapo maneno ambayo baadhi ya wanafunzi walishindwa kuyasoma kutokana na sababu mbalimbali. Maneno hayo ni kama kompyuta (34.64%), mbwa (27.14%), mwanga (23.55%), mwavuli (23.53%) na chumvi (22.04%). Wanafunzi hao walishindwa kusoma neno ‘kompyuta’ kwa sababu lina silabi iliyoundwa na konsonanti pekee ambayo ni ‘m’. Vile vile neno hilo lina silabi yenye muundo wa konsonanti inayoambatana na kiyeyusho ‘y’ chenye sifa ya irabu na irabu ‘u’ “pyu”, hivyo wanafunzi walishindwa kutamka kiyeyusho na irabu kwa wakati mmoja.

Neno ‘mbwa’ lilikuwa na changamoto ya kusomwa kwa sababu halisomwi kama linavyoandikwa kwa kuwa lina konsonanti zinazofanana na zinafuatana hivyo katika matamshi konsonanti moja hudondoshwa. Sauti ‘m’ ya kwanza hutamkwa tu lakini haibainiki katika maandishi. Vilevile, maneno ‘mwanga’ na “mwavuli” yameundwa na silabi zenye mfuatano wa konsonanti ambazo ni ‘mw’ na ‘ng’. Aidha neno “chumvi” lina herufi “m” ambayo ni silabi iliyoundwa na konsonanti pekee na mwanafunzi anaposoma neno hilo hana budi kuisoma kama silabi. Kwa ujumla, maneno yenye silabi zilizoundwa na konsonanti moja na irabu yanasomeka kwa urahisi ikilinganishwa na maneno yenye silabi zenye muundo wa konsonanti zaidi ya moja na irabu.

#### 2.4.1.2 Utendaji wa Wanafunzi Wanaojifunza kwa Lugha ya Kiingereza

Wanafunzi wanaojifunza kwa lugha ya Kiingereza wameonesha utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa asilimia 98.59. Wanafunzi hao waliweza kusoma maneno 7 hadi 25 kwa ufasaha. Hata hivyo, jumla ya wanafunzi 13 sawa na asilimia 1.41 walishindwa kusoma maneno yote na wengine waliweza kusoma maneno pungufu ya 7 na kuwa na utendaji hafifu kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4


**Jedwali Na. 4: Utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Maneno ya Kiingereza**

| Maneno | Utendaji | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 0 – 6 | Hafifu | 13 | 1.41 |
| 7 – 13 | Wastani | 26 | 2.82 |
| 14 – 19 | Mzuri | 72 | 7.80 |
| 20 – 25 | Mzuri Sana | 812 | 87.97 |
| | **Jumla** | **923** | **100.00** |

Matokeo ya uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi yameonesha kuwa, wanafunzi wengi waliweza kusoma baadhi ya maneno kwa usahihi. Maneno hayo ni “dog” (98.37%), “cup” (98.26%), na “pin” (97.18%) ambayo yalisomwa kwa urahisi kwani yameundwa kwa silabi moja (monosyllable). Pia neno “pin” na “dog” yana uhusiano wa moja kwa moja kati ya matamshi na maumbo yake.

Pamoja na wanafunzi kuonesha umahiri wa juu katika kusoma maneno, yapo maneno ambayo baadhi yao walishindwa kuyasoma kwa ufasaha.


Maneno hayo ni “guitar” (31.97%), “computer” (20.92%), “salt” (20.92%), “cock” (16.8%) na “vitamins” (12.9%). Neno “guitar” liliwatatiza wanafunzi wengi kwa sababu herufi “ui” hutamkwa kama sauti moja /i/ ambapo hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya herufi na matamshi. Vile vile neno ‘computer’ lina silabi yenye muundo wa konsonanti iliyoambatana na kiyeyusho (semi-vowel) ‘y’ chenye sifa ya irabu ambacho hutamkwa lakini kwenye maandishi hakionekani. Aidha neno “cock” linapotamkwa herufi “c” hudondoshwa hivyo basi kutokudondosha herufi hiyo kulisababisha neno hilo kutokusomwa kwa ufasaha. Chati Na. 2 inaonesha utendaji hafifu wa wanafunzi kwa kila neno.




**Chati Na. 2:** *Asilimia ya Wanafunzi Walioshindwa Kusoma Maneno ya Kiingereza.*

### 2.4.2 Swali la 2: Umahiri wa Kusoma Sentensi

Katika swali hili mwanafunzi alitakiwa kusoma sentensi tano (5) zenye jumla ya maneno ishirini na tano (25) kwa muda wa dakika moja. Jumla ya wanafunzi 5,088 sawa na asilimia 90.52 walionesha utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa kuweza kusoma kwa ufasaha maneno 7 hadi 25 katika sentensi. Chati Na. 3 inafafanua viwango vya utendaji wa wanafunzi.




**Chati Na. 3**: *Utendaji wa Wanafunzi Katika Kusoma Sentensi.*

Chati Na.3 inaonesha kuwa, wanafunzi 4,627 sawa na asilimia 82.32 walikuwa na utendaji mzuri sana. Wanafunzi hao waliweza kusoma maneno 20 hadi 25 ambayo ni zaidi ya robo tatu ya maneno yote yaliyokuwa katika sentensi walizopewa. Kielelezo Na. 6 ni sampuli ya majibu ya wanafunzi waliokuwa na utendaji mzuri sana.

| 2. Kusoma sentensi (alama 25) | 2. Reading of the sentences (25 marks) |
|---|---|
| Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno katika sentensi ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama** 1) | Put a **stroke mark (/)** in all words in a sentence which the pupil has **failed** to read. Circle **(Ø)** if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed (The score for each correct word is **1 mark**) |
| Mbuzi wangu wana mikia mifupi. | My goats have short tails. |
| Njoo hapa dada yangu mpole. | Come here my calm sister. |
| Tafadhali fungua kitabu chako vizuri. | Please, open your book carefully. |
| Viatu vyangu vyote ni vyeusi. | All my shoes are black. |
| Hawa ni watoto wadogo sana. | These are very young children. |

**Kielelezo Na 6:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno ishirini na tano (25).

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi 291 sawa na asilimia 5.18 walikuwa na utendaji mzuri kwa kuweza kusoma kati ya maneno 14 hadi 19. Maneno hayo ni zaidi ya nusu ya maneno yaliyokuwa katika

sentensi zote tano kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 7.

| 2. Kusoma sentensi (alama 25) | 2. Reading of the sentences (25 marks) |
|---|---|
| Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno katika sentensi ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama** 1) | Put a **stroke mark (/)** in all words in a sentence which the pupil has **failed** to read. Circle **(Ø)** if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed (The score for each correct word is **1 mark**) |
| Mbuzi wangu wana mikia mifupi. | My goats have short tails. |
| Njoo hapa dada yangu mpole. | Come here my calm sister. |
| Tafadhali fungua kitabu chako vizuri. | Please, open your book carefully. |
| Viatu vyangu vyote ni vyeusi. | All my shoes are black. |
| Hawa ni watoto wadogo sana. | These are very young children. |

**Kielelezo Na 7:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno 16.

Vile vile asilimia 3.02 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani kwa kusoma maneno 7 hadi 13 ambayo ni nusu au chini ya nusu ya maneno yote. Kielelezo Na. 8 ni sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji wa wastani.

| 2. Kusoma sentensi (alama 25) | 2. Reading of the sentences (25 marks) |
|---|---|
| Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno katika sentensi ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama** 1) | Put a **stroke mark (/)** in all words in a sentence which the pupil has **failed** to read. Circle **(Ø)** if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed (The score for each correct word is **1 mark**) |
| Mbuzi wangu wana mikia mifupi. | My goats have short tails. |
| Njoo hapa dada yangu mpole. | Come here my calm sister. |
| Tafadhali fungua kitabu chako vizuri. | Please, open your book carefully. |
| Viatu vyangu vyote ni vyeusi. | All my shoes are black. |
| Hawa ni watoto wadogo sana. | These are very young children. |

**Kielelezo Na 8:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma maneno 7 hadi 13.

Wanafunzi 533 sawa na asilimia 9.48 walikuwa na utendaji hafifu. Kati yao, asilimia 3.52 waliweza kusoma kwa ufasaha neno 1 hadi maneno 6 na asilimia 5.96 walishindwa kusoma neno hata moja katika sentensi walizopewa. Wanafunzi hao hawakuwa na umahiri katika stadi ya kusoma kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 9 na 10.

| 2. Kusoma sentensi (alama 25) | 2. Reading of the sentences (25 marks) |
|---|---|
| Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno katika sentensi ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama** 1) | Put a **stroke mark (/)** in all words in a sentence which the pupil has **failed** to read. Circle **(Ø)** if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed (The score for each correct word is **1 mark**) |
| Mbuzi wangu wana mikia mifupi.<br>Njoo hapa dada yangu mpole.<br>Tafadhali fungua kitabu chako vizuri.<br>Viatu vyangu vyote ni vyeusi.<br>Hawa ni watoto wadogo sana. | My goats have short tails.<br>Come here my calm sister.<br>Please, open your book carefully.<br>All my shoes are black.<br>These are very young children. |

**Kielelezo Na 9:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kusoma neno 1 hadi maneno 6

| 2. Kusoma sentensi (alama 25) | 2. Reading of the sentences (25 marks) |
|---|---|
| Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno katika sentensi ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama** 1) | Put a **stroke mark (/)** in all words in a sentence which the pupil has **failed** to read. Circle **(Ø)** if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed (The score for each correct word is **1 mark**) |
| Mbuzi wangu wana mikia mifupi.<br>Njoo hapa dada yangu mpole.<br>Tafadhali fungua kitabu chako vizuri.<br>Viatu vyangu vyote ni vyeusi.<br>Hawa ni watoto wadogo sana. | My goats have short tails.<br>Come here my calm sister.<br>Please, open your book carefully.<br>All my shoes are black.<br>These are very young children. |

**Kielelezo Na 10:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioshindwa kusoma maneno yote katika sentensi walizopewa.

#### 2.4.2.1 Utendaji wa Kusoma Sentensi kwa Wanafunzi Wanaojifunza kwa Lugha ya Kiswahili

Wanafunzi 4,178 sawa na asilimia 88.93 wanaojifunza kwa lugha ya Kiswahili walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika kusoma sentensi walizopewa. Umahiri wao ulitokana na uwezo wa kusoma maneno katika sentensi husika kwa ufasaha, kwa muda wa dakika moja na kwa mtiririko unaoleta mantiki.

Ingawa wanafunzi wengi walikuwa na umahiri wa kusoma sentensi walizopewa, wapo walioshindwa kusoma baadhi ya maneno katika sentensi husika. Kwa mfano, katika sentensi ya kwanza “Mbuzi wangu wana mikia mifupi” asilimia 16.69 ya wanafunzi walishindwa kusoma neno “wangu” na asilimia 16.48 walishindwa kusoma neno “mbuzi”. Wanafunzi walishindwa kusoma maneno hayo kwa sababu yameundwa na silabi zenye mfuatano wa konsonanti mbili na irabu. Kwa mfano, silabi “ngu” katika neno 'wangu' na “mbu” katika neno “mbuzi”.

Hata hivyo, katika sentensi ya pili “Njoo hapa dada yangu mpole”, asilimia 24.97 ya wanafunzi walishindwa kusoma neno 'njoo' kutokana na kuwepo kwa silabi “njo” iliyoundwa na mfuatano wa konsonanti mbili na irabu. Vilevile silabi “o” iliwatatiza wanafunzi wengi kwa sababu ni silabi iliyoundwa na irabu peke yake, hivyo ilisababisha wanafunzi kusoma silabi “njo” na kuacha irabu “o” ambayo imesimama kama silabi katika neno hilo. Aidha asilimia 16.24 walishindwa kusoma neno “mpole” kutokana na kuwepo kwa herufi "m" ambayo imeundwa na konsonanti pekee ambayo wakati wa kusoma husimama kama silabi.


Wanafunzi 3,445 sawa na asilimia 26.67 walishindwa kusoma neno “Tafadhali” katika sentensi ya tatu “Tafadhali fungua kitabu chako vizuri”. Wanafunzi hao walishindwa kusoma neno hilo kwa sababu ya ukaribu wa mahali pa kutamkia sauti “dh” “z”, na “s” ambapo “dh” hutamkwa wakati ncha ya ulimi inapogusana na meno ya juu. Sauti “z” na “s” hutamkwa wakati ncha ya ulimi inapogusana na ufizi. Hivyo baadhi ya wanafunzi walitamka neno “Tafasali/tafazali” badala ya “tafadhali” wakati wa kusoma.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 22.46 ya wanafunzi walishindwa kusoma neno “vyangu”, 22.03 “vyeusi” na 20.84 “vyote” katika sentensi ya nne “Viatu vyangu vyote ni vyeusi”. Wanafunzi hao walishindwa kusoma maneno hayo kwa sababu yana silabi “vya”, “vye” na “vyo” ambazo zimeundwa na konsonanti mwambatano “vy”. Aidha,

sauti /v/ na /f/ ambazo zote zinatamkwa kwa kugusanisha mdomo wa chini na meno ya juu zilichanganywa wakati wa kutamka. Hivyo, wanafunzi wengi walitamka “fyangu” badala ya “vyangu”, “fyeusi” badala ya “vyeusi” na “fyote” badala ya “vyote”.

Uchambuzi zaidi katika kila sentensi unaonesha kuwa, wanafunzi 4,090 sawa na asilimia 87.06 waliweza kusoma vizuri zaidi sentensi ya tano “Hawa ni watoto wadogo sana” kuliko sentensi zingine. Wanafunzi hao waliweza kusoma sentensi hiyo kwa sababu imeundwa kwa maneno ya silabi zenye muundo rahisi wa konsonanti na irabu.


Kwa ujumla, zaidi ya asilimia 82 ya wanafunzi wanaojifunza kwa lugha ya Kiswahili walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana, kwa sababu waliweza kusoma maneno 3 hadi 5 katika kila sentensi. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya utendaji wa wanafunzi katika usomaji wa sentensi ya kwanza hadi ya tano.




**Chati Na. 4:** *Utendaji wa Wanafunzi Katika Usomaji wa Sentensi za Kiswahili.*

### 2.4.2.2 Utendaji wa Kusoma sentensi kwa Wanafunzi Wanaojifunza kwa Lugha ya Kiingereza

Asilimia kubwa ya wanafunzi wanaojifunza kwa lugha ya Kiingereza walikuwa na umahiri wa kutosha katika kusoma sentensi walizopewa. Jumla ya wanafuzi 910 sawa na asilimia 98.59 wameonesha utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya utendaji wa wanafunzi katika kila sentensi.




**Chati Na. 5:** *Utendaji wa Wanafunzi Katika Usomaji wa Sentensi za Kiingereza.*

Pamoja na wanafunzi wengi kuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika usomaji wa sentensi, katika sentensi ya kwanza “My goats have short tails” asilimia 19.07 ya wanafunzi walishindwa kusoma neno 'tails'. Ugumu wa kusoma neno hilo ulitokana na matamshi yake kutokuwa na uhusiano wa moja kwa moja na umbo lake. Kwa mfano, herufi “ai” zinatamkwa /ei/ na “s” inatamkwa /z/ hivyo neno “tails” lilitakiwa kusomwa /teilz/.

Katika sentensi ya pili, "Come here my calm sister", asilimia 25.46 ya wanafunzi walishindwa kusoma neno “calm”. Wakati wa kusoma neno hilo herufi “c” ilitakiwa kutamkwa kama sauti /k/ na sauti /l/ kudondoshwa. Hivyo, neno hilo liliwashinda wanafunzi wengi kuliko maneno yote.

Vilevile wanafunzi 167 sawa na asilimia 18.09 walishindwa kusoma neno “carefully” katika sentensi ya tatu “Please open your book carefully”. Wanafunzi hao walishindwa kusoma neno hilo kwa kuwa matamshi yake hayana uhusiano wa moja kwa moja na umbo la neno. Kwa mfano, herufi “c” ilitakiwa kutamkwa /k/, herufi mbili za “ll” ziliwakilishwa na sauti moja ambayo ni /l/ na sauti /u/ ilitakiwa kudondoshwa wakati wa kusoma.

Katika sentensi ya nne “All my shoes are black” neno ‘all’ lilikuwa na changamoto ya kusomwa kwa asilimia 14.37. Wanafunzi hao walishindwa kusoma neno hilo kwani linaposomwa huanza kwa kutamka

sauti ya irabu inayovutwa (long vowel) ambayo ni ‘a’ pamoja na kudondosha herufi ‘l’ ya mwisho.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 16.79 ya wanafunzi walishindwa kusoma neno “These” katika sentensi “These are my shoes”. Wanafunzi hao walishindwa kubaini muunganiko wa konsonanti mbili ‘th’ ambazo zinatamkwa kama sauti moja. Vile vile herufi ‘s’ ilitakiwa kutamkwa kama sauti ‘z’ na irabu ‘e’ ya mwisho ilipaswa kudondoshwa.

Kwa ujumla katika lugha ya Kiingereza maneno yenye kusomwa kwa irabu za kuvutwa (long vowel), irabu za kudondoshwa pamoja na maneno yasiyo na mahusiano ya moja kwa moja kati ya matamshi na maumbo yake, yameonekana kuwashinda baadhi ya wanafunzi.

### 2.4.3 Swali la 3: Umahiri wa Kujenga Ufahamu Katika Kusoma

Swali hili lilipima umahiri wa mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno na kujibu maswali kwa mdomo. Baada ya mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno alitakiwa kujibu vipengele vinne vya maswali yaliyotokana na maneno aliyoyasoma. Msimamizi alisoma maswali na mwanafunzi alipewa muda wa dakika tatu kujibu. Kifungu cha maneno alichotakiwa kukisoma ni hiki kifuatacho:

> Furaha ana umri wa miaka nane. Anaishi Kinondoni na kaka yake mkubwa. Mara zote hutunza vitu vyake vizuri. Siku ya Jumatatu, Furaha alikwenda dukani kununua penseli. Alikuwa na shilingi mia tano mfukoni. Alinunua penseli mbili kwa shilingi mia nne. Furaha alibaki na shilingi mia moja ambazo alizitumia kununua kifutio.

Kwa upande wa wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza kujifunzia, kifungu hicho kiliandikwa kwa lugha hiyo kama ifuatavyo:

> Furaha is eight years old. She lives at Kinondoni with her elder Brother. She always keeps her things properly. On Monday, Furaha went to the shop to buy pencils. She had five hundred shillings in her pocket. She bought two pencils for four hundred shillings. Furaha remained with one hundred shillings which she used to buy an eraser.

Jumla ya wanafunzi 4,635 sawa na asilimia 82.46 waliweza kujibu kipengele zaidi ya kimoja cha swali hili kwa usahihi na kuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Jedwali Na.5 ni viwango vya utendaji vya wanafunzi hao.

**Jedwali Na. 5: Utendaji wa Wanafunzi katika Kujibu Maswali ya Ufahamu**

| Idadi ya Vipengele | Viwango vya Utendaji | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|---|
| 1 | Hafifu | 986 | 17.54 |
| 2 | Wastani | 633 | 11.26 |
| 3 | Mzuri | 1,372 | 24.41 |
| 4 | Mzuri sana | 2,630 | 46.79 |
| **Jumla** | | **5,621** | **100** |

Uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 2,630 sawa na asilimia 46.79 walikuwa na utendaji mzuri sana. Wanafunzi hao wameonesha umahiri wa juu zaidi katika kujibu maswali ya ufahamu kwa kuweza kujibu vipengele vyote vinne vya swali kwa usahihi. Kielelezo Na.11 ni sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kujibu vipengele vyote vya swali hili.

**Maswali na Majibu**

Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi kuanzia kipengele (a) hadi (c) zungushia alama 3 na kipengle (d) alama $3^1/_2$, iwapo atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama 0 na kisha andika jumla ya alama katika nafasi kwenye jedwali lifuatalo:

| Na | Maswali na majibu | alama | |
|---|---|---|---|
| (a) | Furaha ana umri wa miaka mingapi? (nane) | 3 (circled) | 0 |
| (b) | Furaha anaishi na nani? (kaka yake mkubwa) | 3 (circled) | 0 |
| (c) | Furaha alikwenda wapi siku ya Jumatatu? (dukani) | 3 (circled) | 0 |
| (d) | Furaha alitumiaje shilingi mia tano aliyokuwa nayo? (alinunulia penseli mbili na kifutio) | $3^1/_2$ (circled) | 0 |
| Jumla Alama | | 12½ | |

**Questions and Answers**

If a pupil will give a correct answer, circle 3 marks for letter (a) up to (c) and $3^1/_2$ marks for letter (d), if he/she will give an incorrect answer, circle the 0 mark and then write the total marks in the space provided in the table.

| No. | Question and Answer | Marks | |
|---|---|---|---|
| (a) | How old is Furaha? (Eight years) | 3 (circled) | 0 |
| (b) | Who lives with Furaha? (Her elder brother) | 3 (circled) | 0 |
| (c) | Where did Furaha go on Monday? (To the shop) | 3 (circled) | 0 |
| (d) | How did Furaha spend her five hundred shilings? (She used it to buy two pencils and an eraser) | $3^1/_2$ (circled) | 0 |
| Total | | 12½ | |

**Kielelezo Na 11:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi waliojibu vipengele vinne kwa usahihi

Aidha, wanafunzi 1,372 sawa na asilimia 24.41 waliweza kujibu vipengele vitatu vya swali kwa usahihi na kuwa na utendaji mzuri kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 12.

**Maswali na Majibu**

Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi kuanzia kipengele (a) hadi (c) zungushia alama 3 na kipengle (d) alama $3^1/_2$, iwapo atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama 0 na kisha andika jumla ya alama katika nafasi kwenye jedwali lifuatalo:

| Na | Maswali na majibu | alama | |
|---|---|---|---|
| (a) | Furaha ana umri wa miaka mingapi? **(nane)** | 3 | 0 |
| (b) | Furaha anaishi na nani? **(kaka yake mkubwa)** | 3 | 0 |
| (c) | Furaha alikwenda wapi siku ya Jumatatu? **(dukani)** | 3 | 0 |
| (d) | Furaha alitumiaje shilingi mia tano aliyokuwa nayo? **(alinunulia penseli mbili na kifutio)** | $3^1/_2$ | 0 |
| | **Jumla Alama** | 9 | |

**Questions and Answers**

If a pupil will give a correct answer, circle 3 marks for letter (a) up to (c) and $3^1/_2$ marks for letter (d), if he/she will give an incorrect answer, circle the 0 mark and then write the total marks in the space provided in the table.

| No. | Question and Answer | Marks | |
|---|---|---|---|
| (a) | How old is Furaha? **(Eight years)** | 3 | 0 |
| (b) | Who lives with Furaha? **(Her elder brother)** | 3 | 0 |
| (c) | Where did Furaha go on Monday? **(To the shop)** | 3 | 0 |
| (d) | How did Furaha spend her five hundred shilings? **(She used it to buy two pencils and an eraser)** | $3^1/_2$ | 0 |
| | **Total** | 9 | |

**Kielelezo Na 12:** Majibu ya wanafunzi waliojibu vipengele vitatu vya swali kwa usahihi.

Utendaji wa wastani umeoneshwa na wanafunzi 633 sawa na asilimia 11.26 kwa kuweza kujibu vipengele viwili vya swali kwa usahihi. Kielelezo Na. 13 ni sampuli ya majibu ya wanafunzi hao.

**Maswali na Majibu**

Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi kuanzia kipengele (a) hadi (c) zungushia alama 3 na kipengle (d) alama $3^1/_2$, iwapo atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama 0 na kisha andika jumla ya alama katika nafasi kwenye jedwali lifuatalo:

| Na | Maswali na majibu | alama | |
|---|---|---|---|
| (a) | Furaha ana umri wa miaka mingapi? **(nane)** | 3 | 0 |
| (b) | Furaha anaishi na nani? **(kaka yake mkubwa)** | 3 | 0 |
| (c) | Furaha alikwenda wapi siku ya Jumatatu? **(dukani)** | 3 | 0 |
| (d) | Furaha alitumiaje shilingi mia tano aliyokuwa nayo? **(alinunulia penseli mbili na kifutio)** | $3^1/_2$ | 0 |
| | **Jumla Alama** | 6 | |


**Questions and Answers**

If a pupil will give a correct answer, circle 3 marks for letter (a) up to (c) and $3^1/_2$ marks for letter (d), if he/she will give an incorrect answer, circle the 0 mark and then write the total marks in the space provided in the table.

| No. | Question and Answer | Marks | |
|---|---|---|---|
| (a) | How old is Furaha? **(Eight years)** | 3 | 0 |
| (b) | Who lives with Furaha? **(Her elder brother)** | 3 | 0 |
| (c) | Where did Furaha go on Monday? **(To the shop)** | 3 | 0 |
| (d) | How did Furaha spend her five hundred shilings? **(She used it to buy two pencils and an eraser)** | $3^1/_2$ | 0 |
| | **Total** | 6 | |

**Kielelezo Na 13:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kujibu vipengele viwili vya swali kati ya vinne kwa usahihi na kupata alama za wastani.

Vile vile, uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 986 sawa na asilimia 17.54 walikuwa na utendaji hafifu. Miongoni mwao, wanafunzi 305 sawa na asilimia 5.42 waliweza kujibu kwa usahihi kipengele kimoja tu kati ya vinne na asilimia 12.12 walishindwa kujibu vipengele vyote vya swali. Kielelezo Na.14 kinaonesha majibu ya wanafunzi wenye utendaji hafifu.



Maswali na Majibu

Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi kuanzia kipengele (a) hadi (c) zungushia alama 3 na kipengle (d) alama $3^1/_2$, iwapo atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama 0 na kisha andika jumla ya alama katika nafasi kwenye jedwali lifuatalo:

| Na | Maswali na majibu | alama | |
|---|---|---|---|
| (a) | Furaha ana umri wa miaka mingapi? (nane) | 3 | 0 |
| (b) | Furaha anaishi na nani? (kaka yake mkubwa) | 3 | 0 |
| (c) | Furaha alikwenda wapi siku ya Jumatatu? (dukani) | 3 | 0 |
| (d) | Furaha alitumiaje shilingi mia tano aliyokuwa nayo? (alinunulia penseli mbili na kifutio) | $3^1/_2$ | 0 |
| | Jumla Alama | | 0 |


Questions and Answers

If a pupil will give a correct answer, circle 3 marks for letter (a) up to (c) and $3^1/_2$ marks for letter (d), if he/she will give an incorrect answer, circle the 0 mark and then write the total marks in the space provided in the table.

| No. | Question and Answer | Marks | |
|---|---|---|---|
| (a) | How old is Furaha? (Eight years) | 3 | 0 |
| (b) | Who lives with Furaha? (Her elder brother) | 3 | 0 |
| (c) | Where did Furaha go on Monday? (To the shop) | 3 | 0 |
| (d) | How did Furaha spend her five hundred shilings? (She used it to buy two pencils and an eraser) | $3^1/_2$ | 0 |
| | Total | | 0 |

**Kielelezo Na 14:** Majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu vipengele vyote vya swali hili.

Katika swali hili, utendaji wa juu zaidi umebainika katika kipengele (a) kilichouliza “Furaha ana umri wa miaka mingapi?” Utendaji wa kipengele hiki ulikuwa wa juu kutokana na kupima umahiri wa mwanafunzi katika kukumbuka. Aidha, utendaji wa wastani umebainika katika kipengele (d) kilichouliza, “Furaha alitumiaje shilingi mia tano aliyokuwa nayo?” kwani kipengele hicho kilipima umahiri wa mwanafunzi wa kuchambua. Chati Na. 6 inaonesha asilimia ya utendaji wa wanafunzi katika kila kipengele.




**Chati Na. 6:** *Utendaji wa Wanafunzi kwa Kila Kipengele cha Swali.*

### 2.4.4 Ulinganifu wa utendaji wa Wanafunzi katika Kusoma Sentensi na Kifungu cha Maneno

Jumla ya wanafunzi 4,002 walionesha utendaji mzuri hadi mzuri sana katika kujenga ufahamu wa kusoma na kujibu maswali kwa mdomo. Wanafunzi hao pia walionesha umahiri wa juu katika kusoma sentensi ambapo wanafunzi 3,996 sawa na asilimia 97 walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Ulinganifu huu unaonesha kuwa, wanafunzi wanaoweza kusoma sentensi, wana uwezo wa kusoma kifungu cha maneno, kukielewa na kujibu maswali kwa usahihi.

### 2.4.5 Utendaji wa Wanafunzi Katika Kujenga Ufahamu wa Kusoma Kifungu cha maneno kwa Wanafunzi Wanaotumia Lugha ya Kiswahili Kujifunzia


Uchambuzi unaonesha kuwa, jumla ya wanafunzi 3,811 sawa na asilimia 81.12 walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika kujenga ufahamu wa kusoma. Wanafunzi hao waliweza kujibu vipengele viwili au zaidi vilivyoulizwa kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 6.

**Jedwali Na. 6: Utendaji wa Wanafunzi katika Umahiri wa Kusoma kwa Ufahamu**

| Idadi ya Vipengele | Viwango vya Utendaji | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|---|
| 1 | Hafifu | 887 | 18.88 |
| 2 | Wastani | 506 | 10.77 |
| 3 | Mzuri | 1,078 | 22.95 |
| 4 | Mzuri sana | 2,227 | 47.40 |
| **Jumla** | | **4,698** | **100.00** |

Aidha, utendaji wa wanafunzi katika umahiri wa kusoma kifungu cha maneno na kujibu maswali kwa mdomo kwa kila kipengele unaonesha kuwa, wanafunzi 3,310 sawa na asilimia 70.46 waliweza kujibu kipengele (a) cha swali hili. Swali hilo liliuliza "Furaha ana umri wa miaka mingapi?" Vile vile wanafunzi 3,421 sawa na asilimia 72.82 walijibu kwa usahihi kipengele (b) kilichouliza "Furaha anaishi na nani?" Kipengele (c) ambacho kiliuliza "Furaha alikwenda wapi siku ya Jumatatu?" kilijibiwa kwa usahihi na wanafunzi 3,333 sawa na asilimia 70.95. Aidha jumla ya wanafunzi 3,331 sawa na asilimia 70.90 walijibu kwa usahihi kipengele (d) kilichouliza "Furaha alitumiaje shilingi mia tano aliyokuwa nayo?"

Uchambuzi zaidi wa utendaji wa wanafunzi katika vipengele vya swali hili unaonesha kuwa, kipengele (b) "Furaha anaishi na nani?" kilikuwa na utendaji wa juu zaidi. Wanafunzi wengi (72.82%) walijibu kipengele hicho kwa usahihi kwa sababu swali hili lilipima umahiri wa kukumbuka hivyo, kuweza kujibu kwa urahisi. Chati Na. 7 inaonesha asilimia ya utendaji mzuri wa wanafunzi katika kila kipengele.




**Chati Na. 7:** *Asilimia ya Utendaji wa Wanafunzi Katika kila Kipengele*

Hata hivyo, wapo wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi vipengele vya swali hili ambapo katika kipengele (a) asilimia 29.54 ya wanafunzi walishindwa kujibu kwa usahihi, (b) asilimia 27.18, (c) asilimia 29.05 na (d) asilimia 29.1. Jedwali Na 7 linaonesha asilimia ya wanafunzi walioshindwa kujibu kila kipengele.

**Jedwali Na. 7: Asilimia ya Wanafunzi walioshindwa Kujibu Swali la Ufahamu kwa kila Kipengele**

| Swali | Waliopimwa | Walioshindwa Kujibu | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|---|
| 3 (a) | 4,698 | 1,388 | 29.54 |
| 3 (b) | 4,698 | 1,277 | 27.18 |
| 3 (c) | 4,698 | 1,365 | 29.05 |
| 3 (d) | 4,698 | 1,367 | 29.1 |


### 2.4.6 Utendaji wa Wanafunzi katika Kujenga Ufahamu wa Kusoma Kifungu cha Maneno kwa Wanafunzi wanaojifunza kwa Lugha ya Kiingereza

Uchambuzi wa takwimu za Utendaji wa wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza katika kujifunza unaonesha kuwa, wanafunzi wengi (89.27%) waliweza kuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika umahiri wa kusoma kifungu cha maneno na kujibu maswali kwa mdomo. Wanafunzi hao walijibu kwa usahihi vipengele viwili hadi vinne vya swali kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na. 8: Utendaji wa Wanafunzi katika Kujibu Swali la Ufahamu**

| Idadi ya Vipengele | Viwango vya Utendaji | Idadi ya Wanafunzi | Asilimia ya Wanafunzi |
|---|---|---|---|
| 1 | Hafifu | 99 | 10.73 |
| 2 | Wastani | 127 | 13.76 |
| 3 | Mzuri | 294 | 31.85 |
| 4 | Mzuri sana | 403 | 43.66 |
| **Jumla** | | **923** | **100.00** |

Utendaji wa wanafunzi katika kila kipengele cha swali hili unaonesha kuwa, kipengele (a) kilichouliza “How old is Furaha?” kilijibiwa kwa usahihi na wanafunzi 817 sawa na asilimia 88.52. Utendaji huo mzuri ulitokana na swali hilo kupima uwezo wa wanafunzi kukumbuka. Kipengele (b) kilichouliza “Who lives with Furaha?’’ kilijibiwa kwa usahihi na wanafunzi 699 sawa na asilimia 75.73. Vilevile, kipengele (c) kilichouliza “Where did Furaha go on Monday? kilijibiwa kwa usahihi na wanafunzi 735 sawa na asilimia 79.63. Aidha, kipengele (d) kilichouliza “How did Furaha spend her five hundred shillings?” kilikuwa na utendaji wa asilimia 60.78 ambapo wanafunzi 561 walijibu kwa usahihi. Utendaji wa chini katika swali hili ulitokana na swali hilo kupima uwezo wa wanafunzi wa kuchambua. Chati Na. 8 inaonesha asilimia ya wanafunzi wanaojifunza kwa lugha ya Kiingereza walivyojibu kila kipengele.




**Chati Na. 8:** *Asilimia ya Utendaji wa Wanafunzi Katika kila Kipengele.*


## 2.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia, Mahali Shule ilipo, Jinsi na Shule Zilizopimwa Mwaka 2017 na Kurudia Kupimwa Mwaka 2018

Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi ulifanyika kati ya shule zinazotumia lugha ya Kiswahili kufundishia na zile zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia; shule za mjini na vijijini; wanafunzi wavulana na wasichana na shule 33 zilizofanya upimaji mwaka 2017 na kurudia mwaka 2018.

Lengo la kufanya ulinganifu ni kubaini kama kuna tofauti ya utendaji wa wanafunzi katika makundi hayo ili kuweza kutoa mapendekezo kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.5.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Stadi ya Kusoma kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia

Jumla ya wanafunzi 4,698 walifanya upimaji katika lugha ya Kiswahili na 923 katika lugha ya Kiingereza. Utendaji wa wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza wamekuwa na utendaji mzuri sana kwa asilimia 86.24 ikilinganishwa na asilimia 76.42 ya wanaotumia lugha ya Kiswahili. Chati Na.9 inaonesha ulinganifu wa utendaji huo.





**Chati Na. 9:** *Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Wanaotumia Lugha ya Kiingereza na Kiswahili.*

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza wamekuwa na utendaji wa juu zaidi wakilinganishwa na wa Kiswahili kwa asilimia 9.51. Kwa ujumla matokeo haya hayatofautiani sana na matokeo ya mwaka 2017 ambapo shule zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia zilikuwa na utendaji wa juu zaidi kuliko zinazotumia lugha ya Kiswahili kwa asilimia 8.71.

### 2.5.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Mahali Shule Ilipo

Takwimu zinaonesha kuwa, wanafunzi 4,041 walifanya upimaji wa Stadi ya Kusoma kutoka shule za vijijini na 1,580 kutoka shule za mjini. Ulinganifu wa utendaji umefanyika ili kubaini kama kuna utofauti wa utendaji kati ya wanafunzi hao. Chati Na. 10 inaonesha matokeo ya ulinganifu wa utendaji kati ya wanafunzi wa shule za mjini na vijijini.





**Chati Na. 10:** *Utendaji wa Wanafunzi Wanaosoma Shule za Mjini na Wanaosoma Shule za Vijijini.*

Uchambuzi unaonesha kuwa wanafunzi waliopo shule za mjini wameonesha utendaji mzuri sana wa asilimia 80.38 wakilinganishwa na wa shule za vijijini (72.03%). Hivyo, wanafunzi wanaosoma katika shule za mjini wameonesha utendaji wa juu (ufaulu wa wastani hadi mzuri sana) zaidi kwa asilimia 4.87 wakilinganishwa na wa shule za vijijini.

### 2.5.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi


Jumla ya wanafunzi 5,621 walifanya upimaji wa Stadi ya Kusoma mwaka 2018, miongoni mwao wavulana walikuwa 2,777 na wasichana 2,844. Uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi hao unaonesha kuwa, wasichana walikuwa na utendaji wa asilimia 91.95 ikilinganishwa na wavulana waliokuwa na asilimia 88.44. Wasichana wamekuwa na utendaji wa juu kuliko wavulana kwa asilimia 3.51 kama inavyoonekana katika Chati Na. 11.




**Chati Na. 11:** *Ulinganifu wa Utendaji kati ya Wavulana na Wasichana.*

### 2.5.4 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Shule 66 Zilizopimwa Mwaka 2017 na Mwaka 2018


Jumla ya wanafunzi 6,174 walifanya upimaji wa Stadi ya Kusoma mwaka 2017 ambapo asilimia 90.13 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Aidha wanafunzi 5,621 walifanya upimaji huo mwaka 2018 na kuonesha utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa asilimia 90.22. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 0.09 ikilinganishwa na mwaka 2017. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa mwaka 2018 asilimia 78.03 ya wanafunzi walikuwa na utendaji mzuri sana ambao umepanda kwa 10.88% ikilinganishwa na asilimia 67.15 ya mwaka 2017 kama inavyoonekana katika Chati Na. 12.




**Chati Na. 12**: *Ulinganifu wa Shule Zilizopimwa Mwaka 2017 na 2018.*

### 2.5.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Shule 33 zilizopimwa mwaka 2017 na kupimwa tena 2018

Jumla ya wanafunzi katika shule 33 zilizofanya upimaji mwaka 2017 walikuwa 3,074 na waliofanya upimaji mwaka 2018 walikuwa 2,547. Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi hao umeoneshwa katika Chati Na. 13.




**Chati Na. 13**: *Ulinganifu wa Shule 33 Zilizopimwa Mwaka 2017 na Kupimwa tena 2018.*

Takwimu katika Chati Na. 13 zinaonesha kuwa, shule 33 zilizofanya upimaji mwaka 2017 zilikuwa na utendaji wa juu wa asilimia 69.14 wakati mwaka 2018 zilikuwa na utendaji wa juu wa asilimia 76.38. Aidha, kumekuwa na upungufu wa asilimia 1.91 katika utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na mwaka 2017.

## 2.6 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi ya Kusoma

Kwa ujumla utendaji wa wanafunzi katika Stadi ya Kusoma ulikuwa mzuri kwani asilimia 90.22 waliweza kusoma maneno, sentensi, kifungu cha maneno na kujibu maswali kwa usahihi. Kwa upande mwingine, asilimia 9.78 hawakuwa na umahiri wa kutosha kwa sababu walishindwa kusoma maneno yanayoundwa na silabi zenye muundo wa konsonanti mwambatano, konsonanti iliyoambatana na kiyeyusho, maneno ya Kiingereza ambayo hayana uhusiano wa moja kwa moja kati ya umbo na matamshi yake na kusoma kwa ufahamu kifungu cha maneno kisha kujibu maswali hasa katika maswali yaliyopima nyanja za juu za utambuzi.

# SURA YA TATU

## UPIMAJI WA STADI YA KUANDIKA

### 3.1 Utangulizi

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika Stadi ya Kuandika ulifanyika kwa kuzingatia vigezo vya utendaji wa wanafunzi ili kupima umahiri wao katika kumudu stadi hii. Aidha, ulinganifu wa umahiri katika utendaji wa wanafunzi ulifanyika kwa kuzingatia shule zinazotumia lugha ya Kiswahili na zinazotumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia. Vile vile, uchambuzi ulihusisha ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi katika upimaji wa stadi ya Kuandika kwa mwaka 2017 na 2018. Pia, ulinganifu wa umahiri wa wanafunzi katika kumudu stadi ya Kuandika umefanyika kwa kuzingatia jinsi na mahali shule zilipo (mijini/vijijini).

Viwango vya Utendaji vya wanafunzi katika Stadi ya Kuandika vilikuwa katika makundi manne ambayo ni utendaji hafifu iwapo mwanafunzi alipata alama 0 hadi 12, utendaji wa wastani (alama 13 hadi 25), utendaji mzuri (alama 26 hadi 38) na utendaji mzuri sana (alama 39 hadi 50).

### 3.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kuandika

Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kuandika ilikuwa na maswali matatu. Swali la kwanza lilikuwa na vipengele 10 ambapo mwanafunzi alitakiwa kutambua picha na kuandika majina yanayowakilisha picha hizo (umahiri wa kuunda maneno). Swali la pili lilikuwa na vipengele 10 na lilipima umahiri wa mwanafunzi wa kutambua herufi kubwa na ndogo ambapo mwanafunzi alitakiwa kupigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa. Swali la tatu lilimtaka mwanafunzi kuandika kwa hisia na uasili kwa kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi.

Karatasi ya upimaji wa Stadi ya Kuandika iliandaliwa kwa lugha ya Kiswahili kwa shule zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia. Karatasi hii ilitafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza kwa shule zinazotumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia.

### 3.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi ya Kuandika kwa kila Umahiri

Umahiri wa mwanafunzi katika stadi ya Kuandika ulipimwa kwa kuzingatia uwezo wao wa kutambua picha na kuandika majina yanayowakilisha picha hizo (umahiri wa kuunda maneno). Umahiri wa mwanafunzi ulikuwa hafifu ikiwa aliweza kuandika majina ya picha 1 - 2, wastani majina ya picha 3 - 5, mzuri majina ya picha 6 - 8 na mzuri sana majina ya picha 9 – 10. Aidha,

umahiri wa mwanafunzi katika kutambua herufi kubwa, ulikuwa hafifu iwapo alipigia mstari maneno 1 - 2, wastani (3 – 5), mzuri (6 – 8) na mzuri sana (9 – 10). Pia, umahiri wa mwanafunzi wa kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi kwa hisia na uasili ulikuwa hafifu ikiwa mwanafunzi alinakili maneno na kuweka alama za uandishi na kupata alama 1 - 5, wastani (6 – 10), mzuri (11 – 15) na mzuri sana (16 – 20).

## 3.4 Uchambuzi wa Takwimu za Majibu ya Wanafunzi

Uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi unaonesha kuwa, wanafunzi 5,677 walifanya upimaji katika stadi ya Kuandika. Muhtasari wa utendaji wa jumla katika stadi ya Kuandika umeoneshwa katika Jedwali Na. 9.


**Jedwali Na. 9: Utendaji wa Jumla wa Stadi ya Kuandika**

| Umahiri | Viwango vya Utendaji | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hafifu | | Wastani | | Mzuri | | Mzuri Sana | |
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| Kuunda Maneno | 612 | 10.78 | 929 | 16.37 | 2,603 | 45.85 | 1533 | 27.00 |
| Matumizi ya Herufi Kubwa na Ndogo | 1,324 | 23.32 | 336 | 5.94 | 594 | 10.46 | 3422 | 60.28 |
| Kunakili Kifungu na Kuweka Alama za Uandishi | 1,209 | 21.30 | 523 | 9.21 | 1,542 | 27.16 | 2,403 | 42.33 |

Jedwali Na. 9 linaonesha utendaji wa wanafunzi ambapo asilimia 89.22, 76.68 na 78.7 walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika umahiri wa kuandika majina ya picha, kutambua herufi kubwa na ndogo na kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi mtawalia. Wanafunzi hao waliweza kutambua picha 3 - 10 na kuandika majina ya picha hizo, kutambua herufi kubwa 3 – 10, kunakili maneno 6 - 16 na kuweka alama za uandishi 2 – 4 katika kifungu cha maneno.


### 3.4.1 Utendaji wa Wanafunzi Katika Kutambua Picha na Kuandika Jina la Picha Husika

Uchambuzi uliofanyika ili kubaini umahiri wa wanafunzi katika kuandika majina ya picha unaonesha kuwa, baadhi ya wanafunzi (45.85%) walikuwa na utendaji mzuri katika dhana ya utambuzi wa picha na kuandika kwa usahihi majina ya picha hizo kama inavyoonekana katika Chati Na. 14.





**Chati Na. 14:** *Utendaji wa Wanafunzi katika Kuandika Majina ya Picha.*

Chati Na. 14 inaonesha utendaji wa wanafunzi katika kuandika majina ya picha ambapo asilimia 89.21 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Aidha, wanafunzi wachache (10.78%) walikuwa na utendaji hafifu. Kielelezo Na. 15 kinaonesha utendaji wa wanafunzi waliokuwa na umahiri wa kutambua picha na kuandika majina katika picha zote.




**Kielelezo Na 15:** Majibu ya wanafunzi walioweza kuandika majina ya picha kwa usahihi.

Asilimia 10.78 ya wanafunzi waliokuwa na utendaji hafifu hawakuwa na umahiri wa kutambua picha na kuandika majina yanayowakilisha picha hizo kwa usahihi. Baadhi ya wanafunzi waliokuwa na utendaji hafifu walishindwa kuandika neno hata moja linalowakilisha picha husika. Wengine waliweza kuandika jina moja hadi mawili tu kutokana na changamoto ya kuunganisha herufi ili kuunda jina sahihi au kuandika baadhi ya majina kwa kukosea herufi (tahajia). Kielelezo Na. 16 kinaonesha sampuli za majibu ya wanafunzi waliokuwa na utendaji hafifu.




**Kielelezo Na 16:** Majibu ya wanafunzi walioshindwa kuandika majina ya picha kwa usahihi.

### 3.4.1.1 Uchambuzi wa Utendaji wa Wanafunzi katika Kutambua na Kuandika Jina la Picha

#### (a) Kisu /Knife

Wanafunzi 3,737 sawa na asilimia 78.59 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia waliandika kwa usahihi jina “kisu”. Wanafunzi hao walionesha kuwa na umahiri wa kutambua picha na kuhusianisha jina sahihi linalowakilisha picha husika. Pia, uchambuzi ulibaini kuwa, jumla ya wanafunzi 1,017 sawa na asilimia 21.39 hawakuweza kutambua picha na kuandika jina la picha husika.

Aidha, uchambuzi uliofanywa kwa wanafunzi kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia

umeonesha kuwa, wanafunzi 666 sawa na asilimia 72.23 waliandika kwa usahihi jina "knife". Wanafunzi 256 (27.77%) walishindwa kuandika tahajia ya neno “knife” na hivyo kuandika kwa kutumia silabi za Kiswahili “naifi”.

**(b) Pikipiki / Motorcycle**

Wanafunzi 3,781 sawa na asilimia 79.52 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia waliandika jina "pikipiki" kwa usahihi. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa wanafunzi 974 (20.48%) walishindwa kuandika jina “pikipiki” kwa usahihi. Baadhi yao waliandika majina yasiyohusiana na picha hiyo kama vile “chungwa” na wengine hawakuandika kitu chochote.

Wanafunzi wachache 132 (14.32%) kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia waliweza kuandika jina "motorcycle" kwa usahihi. Wanafunzi hao walionesha umahiri wa kuhusianisha picha na jina. Aidha, wanafunzi 790 sawa na asilimia 85.68 walishindwa kuandika jina “motorcycle” kwa kukosa stadi ya kuandika konsonanti “cycl” zinazofuatana katika jina hilo. Wanafunzi wengine waliandika jina “mottc”, “motocyocl” na "pikipiki" kwa Kiswahili jambo linaloonesha kuwa hawakuwa na umahiri wa kuandika neno husika.

**(c) Helikopta / Helicopter**

Uchambuzi wa utendaji wa wanafunzi kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia unaonesha kuwa, wanafunzi wengi (98.82%) walishindwa kuandika jina “helikopta” kwa usahihi. Wanafunzi hao walionesha kukosa umahiri wa kutofautisha ndege ya abiria yenye mabawa na yenye panka/pangaboi kwa juu na yenye uwezo wa kutua popote. Aidha, wanafunzi wachache (1.18%) waliweza kutambua picha na kuandika jina kwa usahihi.

Wanafunzi 68 sawa na asilimia 7.38 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia waliweza kuhusisha picha na jina "helicopter" na namna linavyoandikwa kwa usahihi. Aidha, wanafunzi 854 (92.62%) walishindwa kuandika neno "helicopter" ambapo baadhi yao waliandika “helicopta” na wengine waliandika silabi zisizokuwa na maana

kama vile “arecopite” na “eroplan”. Wanafunzi hao, hawakuwa na umahiri wa kuhusisha miundo ya silabi za maneno katika lugha ya Kiingereza na kuandika majina hayo kwa muundo wa silabi za lugha ya Kiswahili.

**(d) Chupa / Bottle**

Takwimu zinaonesha kuwa, wanafunzi wapatao 3,779 sawa na asilimia 79.47 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia waliweza kuandika jina “chupa” kwa usahihi. Wanafunzi hao wameonesha umahiri wa kutambua silabi zinazoundwa kwa konsonanti /ch/ na irabu /u;a/ kwa kuunda neno “chupa”. Aidha, wanafunzi 976 sawa na asilimia 20.53 hawakuwa na umahiri wa kuandika jina “chupa” kama ilivyotakiwa. Kwa mfano, baadhi waliandika neno “huba”, “cupa”, “ukpa” na wengine waliacha sehemu hiyo wazi bila kuandika kitu chochote.

Uchambuzi zaidi umebaini kuwa, wanafunzi 478 sawa na asilimia 51.84 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia walionesha kuwa na umahiri wa kuhusisha maneno ambayo huandikwa kama yanavyotamkwa katika lugha ya Kiingereza. Aidha, jumla ya wanafunzi 444 (48.16%) walishindwa kuandika kwa usahihi jina "bottle" kwani hawakuweza kubaini kuwa jina hilo linaandikwa kama linavyotamkwa na wengine walionesha kuwa na athari ya lugha mama. Hivyo waliandika maneno yasiyo sahihi kama “bottl” “botlo” na botlob” yasiyo sahihi.

**(e) Jongoo/Millipede**

Utendaji wa wanafunzi 2,260 sawa na asilimia 47.53 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia waliweza kuandika neno “jongoo”. Wanafunzi 2,495 sawa na asilimia 52.47 waliandika maneno kama vile "yoka" na “jongo” badala ya kuandika jina "jongoo". Wanafunzi hao hawakuwa na umahiri wa kutambua aina za wadudu na hivyo kushindwa kuandika jina “jongoo” kama picha ilivyokuwa inaonekana.

Utendaji wa wanafunzi 876 (95.01%) katika kuandika jina “millipede” ulikuwa hafifu kutokana na kukosa umahiri wa kuhusisha matamshi na muundo wa silabi za neno "millipede." Aidha, athari za lugha ya Kiswahili na lugha mama zilichangia

wanafunzi hao kuwa na utendaji hafifu. Wanafunzi hao waliandika maneno kama vile "ontho", “andana”, “milipadi” na “kef”. Hata hivyo, wanafunzi wachache (46) sawa na asilimia 4.99 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia waliweza kuandika kwa usahihi jina "millipede". Wanafunzi hao wameonesha kuwa na maarifa ya kuhusisha matamshi na uandishi wa jina “millipede”.

**(f) Kuku/Hen**

Uchambuzi unaonesha kuwa, wanafunzi 4,202 sawa na asilimia 88.37 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia walikuwa na utendaji mzuri katika kuunda herufi za neno “kuku”. Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa kuhusisha picha na kuunda herufi/silabi zinazounda neno “kuku”. Aidha, jumla ya wanafunzi 553 (11.63%) hawakuweza kuandika neno “kuku” kwa usahihi. Wanafunzi hao walionesha kukosa umahiri wa kuhusisha picha na kuunda herufi/silabi za neno “kuku” na kuandika maneno yasiyo sahihi kama “kuki” “kiki” na “kijahi”.

Kwa upande wa wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiingereza kujifunzia na kufundishia, wanafunzi 843 sawa na asilimia 91.43 walionesha umahiri wa juu katika kuhusianisha picha husika na hivyo kuandika kwa usahihi neno "hen".

Takwimu pia zinaonesha wanafunzi 79 sawa na asilimia 8.57 hawakuwa na umahiri katika kuandika jina "hen" kwa usahihi. Baadhi ya wanafunzi waliandika maneno "heni" na "kuku” jambo linaloonesha kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu tahajia za maneno mbalimbali ya Kiingereza na wengine waliathiriwa na lugha ya Kiswahili. Pia, wapo wanafunzi walioacha sehemu hiyo wazi bila kuandika kitu chochote.

**(g) Kitabu/Book**

Jumla ya wanafunzi 3,825 sawa na asilimia 80.44 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia walikuwa na umahiri mzuri katika kuandika jina "kitabu". Wanafunzi hao waliweza kutambua picha na kufahamu namna ya kuandika jina la picha husika kwa usahihi. Aidha, wanafunzi 930

sawa na asilimia 19.56 hawakuwa na umahiri wa kuandika jina sahihi linalowakilisha picha husika.

Uchambuzi zaidi umebainisha kuwa, wanafunzi 853 sawa na asilimia 92.52 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia walikuwa na umahiri mzuri kwa kuweza kutambua picha husika na kuandika kwa usahihi jina "book". Vile vile, wanafunzi 69 sawa na asilimia 7.48 walikosa umahiri wa kuandika jina sahihi la picha husika “book” kutokana na kushindwa kuunda herufi za jina hilo na wengine hawakuandika kitu chochote kuhusu picha hiyo.

**(h) Kinyonga/Chameleon**

Wanafunzi wapatao 2,899 sawa na asilimia 60.97 wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia walikuwa na umahiri mzuri katika kuandika jina "kinyonga". Wanafunzi hao waliweza kutambua picha husika na kuhusianisha na herufi za neno katika kuandika jina la picha hiyo. Pia, wanafunzi 1,856 ambao ni asilimia 39.03 hawakuwa na umahiri mzuri kuhusu jina la picha husika. Wanafunzi hao hawakuweza kutambua majina ya viumbe mbalimbali, hivyo waliandika majina yasiyo sahihi kama vile “manjano”, “mjusi” na “panyabuku”.

Katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia takwimu zinaonesha kuwa, wanafunzi 75 sawa na asilimia 8.13 walikuwa na umahiri katika kuandika jina "chameleon". Aidha, wanafunzi waliokosa umahiri katika kuandika jina hilo walikuwa 847 sawa na asilimia 91.87. Wanafunzi hao hawakuweza kutambua jina linalohusiana na picha husika.

**(i) Panya/Rat**

Katika shule zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia, wanafunzi 3,456 (72.68%) walikuwa na umahiri mzuri katika kuandika jina "panya". Wanafunzi hao waliweza kutambua picha husika na kuandika jina linalohusiana na picha hiyo. Aidha, wanafunzi 1,299 (27.32%) hawakuwa na umahiri katika kuandika jina lililohusiana na picha hiyo. Wanafunzi hao waliandika majina kama vile "saa", “swai” “swala” na wengine hawakuandika kitu chochote.

Kwa upande wa wanafunzi kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia, wanafunzi 789 sawa na asilimia 85.57 walikuwa na umahiri katika kuandika jina “rat”. Wanafunzi hao waliweza kutambua na kuandika jina la picha ya mnyama huyo. Takwimu pia zinaonesha wanafunzi 133 (14.43%) hawakuweza kuandika jina "rat" kutokana na kukosa uelewa wa kuunda herufi za jina husika. Baadhi yao waliandika majina kama “cat”, “lat” na “mice” yasiyo sahihi kulingana na picha husika.


**(j) Samaki/Fish**

Idadi ya wanafunzi 4,058 sawa na asilimia 85.34 wanaotoka katika shule zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kufundishia na kujifunzia walikuwa na umahiri katika kuandika jina "samaki". Aidha, wanafunzi wapatao 697 sawa na asilimia 14.66 hawakuwa na umahiri katika kuandika jina "samaki" kutokana na kushindwa kutambua picha husika na kuihusisha na jina lake. Hivyo waliandika majina kama vile "mkuki" na "semani" ilihali wengine hawakuandika kitu chochote.

Uchambuzi zaidi ulibainisha kuwa, wanafunzi 880 sawa na asilimia 95.44 kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia walikuwa na umahiri mzuri katika kuandika jina "fish". Wanafunzi hao waliweza kutambua viumbe wanaoishi majini na hivyo kuunda herufi sahihi za jina husika. Vile vile, wanafunzi 42 sawa na asilimia 4.56 hawakuwa na umahiri katika kuandika kwa usahihi jina hilo. Wanafunzi hao walishindwa kuunda herufi za jina husika kwa kuwa waliathiriwa na lugha ya Kiswahili, hivyo kuandika majina yasiyo sahihi kama vile "fsh" na "samaki".


### 3.4.2 Umahiri wa Wanafunzi katika Kutambua Herufi Kubwa

Uchambuzi ulifanyika kwa lengo la kubaini umahiri wa wanafunzi katika kutambua herufi kubwa na ndogo. Wakati wa upimaji wa Stadi ya Kuandika, wanafunzi walitakiwa kupigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa. Wanafunzi wengi (76.68%) walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwani walibainisha kwa usahihi herufi kubwa katika maneno waliyopewa. Utendaji wa wanafunzi katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 15.




**Chati Na. 15:** *Utendaji wa wanafunzi katika kutambua herufi kubwa*

Chati Na. 15 inaonesha asilimia 5.94 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani ambapo walibainisha kwa usahihi maneno 3 – 5, asilimia 10.46 utendaji mzuri (maneno 6 – 8) na asilimia 60.28 utendaji mzuri sana (maneno 9 – 10). Miongoni mwao, wapo wanafunzi walioweza kubainisha maneno yote yenye herufi kubwa kwa usahihi kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 16.




2. Pigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa.
   (a) MKATE, chungwa, mlima, KIJIKO
   (b) BLUU, kijani, NYEKUNDU, manjano
   (c) SAA, mkuki, CHAKI, karatasi
   (d) Paka, SIMBA, pundamilia, NYANI
   (e) SHATI, sketi, GAUNI, suruali

2. Underline the words which are written in capital letters.
   (i) BREAD, orange, mountain, SPOON
   (ii) BLUE, green, RED, yellow
   (iii) WATCH, spear, CHALK, paper
   (iv) Cat, LION, zebra, MONKEY
   (v) SHIRT, skirt, DRESS, trousers

**Kielelezo Na 17:** Majibu ya Wanafunzi waliopigia mistari kwa usahihi maneno yote yaliyoundwa kwa herufi kubwa.

Aidha, asilimia 23.32 walikuwa na utendaji hafifu kwani walishindwa kutofautisha maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa na ndogo. Miongoni mwao, wapo wanafunzi ambao hawakupigia mstari neno lolote, na wengine walipigia mstari maneno yenye herufi ndogo au kupigia mstari maneno yote yaliyoandikwa kwa herufi kubwa na ndogo kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 18 na 19.



2. Pigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa.

(a) MKATE, chungwa, mlima, KIJIKO
(b) BLUU, kijani, NYEKUNDU, manjano
(c) SAA, mkuki, CHAKI, karatasi
(d) Paka, SIMBA, pundamilia, NYANI
(e) SHATI, sketi, GAUNI, suruali

2. Underline the words which are written in capital letters.

(i) BREAD, orange, mountain, SPOON
(ii) BLUE, green, RED, yellow
(iii) WATCH, spear, CHALK, paper
(iv) Cat, LION, zebra, MONKEY
(v) SHIRT, skirt, DRESS, trousers

**Kielelezo Na 18:** Majibu ya Wanafunzi waliopigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi ndogo au kupigia mstari maneno yote.


1. Pigia mstari maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa

(a) MKATE, chungwa, mlima, KIJIKO
(b) BLUU, kijani, NYEKUNDU, manjano
(c) SAA, mkuki, CHAKI, karatasi
(d) Paka, SIMBA, pundamilia, NYANI
(e) SHATI, sketi, GAUNI, suruali

1. Underline the words which are written in capital letters.

(i) BREAD, orange, mountain, SPOON
(ii) BLUE, green, RED, yellow
(iii) WATCH, spear, CHALK, paper
(iv) Cat, LION, zebra, MONKEY
(v) SHIRT, skirt, DRESS, trousers

**Kielelezo Na 19:** Majibu ya Wanafunzi ambao hawakupigia mstari neno lolote.


### 3.4.3 Umahiri wa Kunakili Kifungu cha Maneno na Kuweka Alama za Uandishi

Uchambuzi ulilenga kubaini umahiri wa mwanafunzi katika kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama ya nukta (.), mkato (,), kushangaa (!) na kuuliza (?) katika nafasi husika. Umahiri wa wanafunzi katika kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi ulikuwa wa juu kwani asilimia 78.7 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Wanafunzi hao waliweza kunakili maneno na kutumia alama za uandishi kwa usahihi katika kifungu cha maneno. Jedwali Na. 10 linaonesha muhtasari wa utendaji wa wanafunzi.

**Jedwali Na. 10: Umahiri wa Wanafunzi wa Kunakili na Kutumia Alama za Uandishi**

| Idadi ya Wanafunzi | Asilimia | Viwango vya Utendaji |
|---|---|---|
| 1,209 | 21.30 | Hafifu |
| 5,23 | 9.21 | Wastani |
| 1,542 | 27.16 | Mzuri |
| 2,403 | 42.33 | Mzuri sana |

Umahiri wa wanafunzi katika kunakili na kuweka alama za uandishi katika kifungu cha maneno unaonesha kuwa, asilimia 78.7 ya wanafunzi waliojibu swali hili walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Miongoni mwao, asilimia 9.21 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani (maneno 6 – 10), (27.16%) walikuwa na utendaji mzuri (maneno 11 - 15) na (42.33%) walikuwa na utendaji mzuri sana (maneno 16 – 20). Wanafunzi hao walikuwa na umahiri wa juu wa kuunda maneno na kutumia alama za uandishi kwa usahihi na hivyo kuweza kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 20.


3. **Nakili** kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: **nukta** (.), **mkato** (,), **alama ya kushangaa** (!), na **alama ya kuuliza** (?) mahali panapostahili.

Jamani eeh__ Basi la kwenda nyumbani kwetu limetuacha__ Sasa je__ tutaondoka na usafiri wa basi gani__

Jamani eeh! Basi la kwenda nyumbani kwetu limetuacha. Sasa je, tutaondoka na usafiri wa basi gani?


3. **Copy** the following paragraph in the space given and then put the punctuation marks: **full stop** (.), **comma** (,) **exclamation mark** (!) and **question mark** (?) where necessary.

My goodness __ The bus has already left __ So __ which bus are we going to travel by __

My goodness! The bus has already left. So, which bus are we going to travel by?

**Kielelezo Na 20:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi walioweza kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi kwa usahihi.

Kwa upande mwingine, wanafunzi 1,209 sawa na asilimia 21.30 walikuwa na utendaji hafifu kwani walishindwa kunakili kifungu cha maneno na kutumia alama za uandishi kwa usahihi. Baadhi yao hawakunakili kifungu cha maneno na badala yake waliweka alama za uandishi kwenye nafasi zilizoachwa wazi na kunakili alama za uandishi kama Kielelezo Na. 21 kinavyoonesha.




3. **Nakili** kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: **nukta (.)**, **mkato (,)**, **alama ya kushangaa (!)**, na **alama ya kuuliza (?)** mahali panapostahili.

Jamani eeh. Basi la kwenda nyumbani kwetu limetuacha, Sasa je? tutaondoka na usafiri wa basi gani!

. nukta
, Mkato
? Alama ya Kuuliza
)) )) funga nafungua semi

**Kielelezo Na 21:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweka alama za uandishi katika kifungu cha maneno na kunakili majina ya alama za uandishi.

Aidha, wanafunzi wengine walitunga sentensi zisizo na uhusiano na kifungu cha maneno walichopewa kama Kielelezo Na. 22 kinavyoonesha.



3. **Copy** the following paragraph in the space given and then put the punctuation marks: **full stop (.), comma (,) exclamation mark (!)** and **question mark (?)** where necessary.

My goodness __ The bus has already left __ So __ which bus are we going to travel by __

What is your name
I havepen book and bag
Help! Help
I go to School?

**Kielelezo Na 22:** Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyetunga maelezo binafsi yasiyo na uhusiano na kifungu cha maneno.

Uchambuzi zaidi uliofanyika kwa lengo la kubaini umahiri wa wanafunzi wa kutumia alama za uandishi unaonesha kuwa, wanafunzi wachache (35%) waliweka alama ya uandishi katika kifungu cha maneno kwa usahihi. Asilimia 65 ya wanafunzi walishindwa kuweka alama za uandishi kwa usahihi ambapo baadhi ya wanafunzi walitumia alama ya mkato (,) mahali pa kuweka alama ya mshangao (!), alama ya kuuliza (?) mahali pa nukta (.) na kinyume chake. Aidha, alama ya mkato ilikuwa na utendaji wa chini zaidi (74.6%) ikilinganishwa na alama nyingine. Kielelezo Na. 23 kinaonesha utendaji wa wanafunzi waliochanganya matumizi ya alama za uandishi katika kifungu cha maneno.



3. Nakili kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: **nukta (.)**, **mkato (,)**, **alama ya kushangaa (!)**, na **alama ya kuuliza (?)** mahali panapostahili.

Copy the following paragraph in the space given and then put the punctuation marks: **full stop (.)**, **comma (,)** **exclamation mark (!)** and **question mark (?)** where necessary.

Jamani eeh__ Basi la kwenda nyumbani kwetu limetuacha__ Sasa je__ tutaondoka na usafiri wa basi gani__

My goodness __ The bus has already left __ So __ which bus are we going to travel by __

Jamanieeh, Basi lakwenda nyumbani kwetu limetuacha! sasaje? tutaondoka nausafiri Wabasi gani.

My goodness, The bus has already left? So.Which bus are we going to travel by!


**Kielelezo Na 23:** Sampuli ya majibu ya wanafunzi waliotumia alama za uandishi mahali pasipokuwa sahihi katika kifungu cha maneno.

## 3.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia, Mahali Shule ilipo Utendaji wa wanafunzi mwaka 2017 na 2018, Shule 33 Zilizofanya Upimaji Mwaka 2017 na Kurudia 2018

Ulinganifu ulifanyika kwa lengo la kubaini wanafunzi wenye umahiri zaidi kwa kuzingatia lugha ya kufundishia (Kiswahili na Kiingereza), mahali shule ilipo (mjini na vijijini), utendaji wa wanfunzi mwaka 2017 na 2018 na Shule 33 zilizofanya upimaji 2017 na kurudia 2018. Aidha, ulinganifu huu unalenga kubaini changamoto zilizojitokeza ili kutoa mapendekezo ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi ya Kuandika.

### 3.5.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia

Ulinganifu wa umahiri wa wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza ulifanyika. Muhtasari wa taarifa ya ulinganifu umeoneshwa katika Chati Na. 16**.**




**Chati Na. 16:** *Utendaji wa wanafunzi katika Stadi ya Kuandika kwa shule zinazotumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza.*

Chati Na. 16 inaonesha kuwa asilimia 87.80 ya wanafunzi waliofanya upimaji walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika shule zinazotumia lugha ya Kiswahili. Katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza asilimia 96.31 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana.


Hivyo, wanafunzi kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza walikuwa na kiwango kizuri zaidi cha utendaji kwa asilimia 8.51 ikilinganishwa na wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiswahili kufundishia.

### 3.5.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Shule za Mijini na Vijijini

Upimaji wa Stadi ya Kuandika ulihusisha wanafunzi 4,073 kutoka shule za mijini na 1,604 kutoka shule za vijijini. Ulinganifu wa utendaji umefanyika ili kubaini kama kuna tofauti ya utendaji kati ya wanafunzi wa mijini na vijijini. Matokeo ya ulinganifu huu yameoneshwa katika Jedwali Na. 11 na Chati Na. 17.

**Jedwali Na. 11: Ulinganifu wa Utendaji kwa Shule za Mijini na Vijijini**

| Alama | Utendaji | Mijini | | Vijijini | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| 1 - 12 | Hafifu | 390 | 9.58 | 224 | 13.97 |
| 13 - 25 | Wastani | 593 | 14.56 | 263 | 16.40 |
| 26 - 38 | Mzuri | 1,367 | 33.56 | 525 | 32.73 |
| 39 - 50 | Mzuri sana | 1,723 | 42.30 | 592 | 36.91 |




**Chati Na. 17:** *Ulinganifu wa Utendaji wa wanafunzi kutoka shule za Mjini na Vijijini.*

Jedwali Na. 11 na Chati Na. 17 zinaonesha kuwa, wanafunzi wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa shule za mijini ni asilimia 90.42 na kwa shule za vijijini ni asilimia 86.04. Hii inaonesha kuwa, wanafunzi wanaotoka shule za mijini wana utendaji mzuri zaidi ikilinganishwa na wanafunzi wanaotoka shule za vijijini. Matokeo haya yametofautiana na matokeo ya upimaji uliofanyika mwaka 2017 ambapo asilimia 89.57 ya wanafunzi kutoka shule za vijijini walikuwa na utendaji mzuri zaidi ukilinganisha na asilimia 88.38 ya wanafunzi kutoka shule za mijini.

### 3.5.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi Waliofanya Upimaji mwaka 2017 Ikilinganishwa na Mwaka 2018

Jumla ya wanafunzi 5,677 kutoka shule 66 walifanya upimaji mwaka 2018 ambapo mwaka 2017 idadi yao ilikuwa 6,174. Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi hao kwa miaka hiyo miwili umeoneshwa katika Jedwali Na.12.


**Jedwali Na. 12: Ulinganifu wa Utendaji wa wanafunzi waliofanya Upimaji mwaka 2017 na 2018.**

| **Waliopimwa** | | **Wanafunzi Waliopata Utendaji wa Wastani hadi Mzuri Sana** | | | | Ongezeko |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2017 | 2018 | 2017 | | 2018 | | |
| Idadi | Idadi | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | |
| 6,174 | 5,677 | 5,486 | 88.86 | 5,063 | 89.18 | 0.32 |

Jedwali Na. 12 linaonesha kuwa, utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa wanafunzi waliopimwa mwaka 2017 ulikuwa asilimia 88.86 na mwaka 2018 ulikuwa asilimia 89.18. Takwimu hizo zinaonesha kuwa utendaji kwa wanafunzi umeonezeka kwa asilimia 0.32.

### 3.5.4 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Shule 33 Zilizopimwa mwaka 2017 na Kupimwa kwa mara nyingine 2018

Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi wa shule 33 zilizopimwa mwaka 2017 na kufanya upimaji kwa mara ya pili mwaka 2018 umefanyika. Matokeo ya ulinganifu wa utendaji wao yameoneshwa katika Chati Na. 18.




**Chati Na. 8:** *Matokeo ya ulinganifu wa shule 33 zilizopimwa mwaka 2017 na 2018*

Takwimu za ulinganifu katika Chati Na. 18 zinaonesha kuwa, asilimia 91.19 ya wanafunzi waliopimwa mwaka 2017 walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Mwaka 2018 utendaji wa wastani hadi mzuri sana ulikuwa ni wa asilimia 88.06. Hivyo utendaji kwa shule hizo umeshuka kwa asilimia 3.13 kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na mwaka 2017.

### 3.5.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Jinsi

Wanafunzi 5,674 walifanya upimaji katika stadi ya Kuandika mwaka 2018. Miongoni mwao, wanafunzi 2,816 walikuwa wavulana na 2,861 walikuwa wasichana. Jedwali Na. 13 linaonesha ulinganifu wa utendaji wao.

**Jedwali Na. 13: Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Jinsi**

| Alama | Wavulana | | Wasichana | |
|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| **0 -12** | 369 | 13.10 | 245 | 8.56 |
| **13 - 25** | 432 | 15.34 | 425 | 14.85 |
| **26 - 38** | 961 | 34.13 | 930 | 32.51 |
| **39 - 50** | 1,054 | 37.43 | 1,261 | 44.08 |

Jedwali Na. 13 linaonesha kuwa, wasichana walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana wa asilimia 91.44 ikilinganishwa na utendaji wa wavulana wa asilimia 86.9. Hivyo, wasichana walikuwa na utendaji mzuri zaidi wa asilimia 4.54.

## 3.6 Muhtasari wa Uchambuzi katika Stadi ya Kuandika

Takwimu zinaonesha kuwa, wanafunzi wengi (89.18%) walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika mahiri zilizopimwa. Umahiri wa kutambua picha na kuandika majina ya picha ulikuwa na utendaji mzuri zaidi ukilinganishwa na umahiri wa kutofautisha herufi kubwa na ndogo na umahiri wa kuandika kwa hisia na uasili.

Katika umahiri wa kutambua picha na kuandika majina ya picha, asilimia 89.22 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwani waliweza kuandika majina sahihi ya picha 3 hadi 10. Kwa upande wa umahiri wa kutofautisha herufi kubwa na ndogo, asilimia 76.68 ya wanafunzi walionesha utendaji wa wastani hadi mzuri sana wa kutambua herufi kubwa kwani waliweza kupigia mstari maneno 3 hadi 10 kwa usahihi.

Aidha, katika umahiri wa kuandika kwa hisia na uasili, asilimia 78.7 ya wanafunzi waliweza kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi ambapo walinakili maneno 6 hadi 16 ya kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi 2 hadi 4 kwa usahihi.

# SURA YA NNE

## UPIMAJI WA STADI YA KUHESABU

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua muundo wa karatasi ya upimaji, vigezo vya kupima umahiri wa wanafunzi katika Stadi ya Kuhesabu na uchambuzi wa majibu ya wanafunzi. Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa kuzingatia lugha ya kujifunzia na kufundishia, mahali shule ilipo, jinsi na shule zilizopimwa mwaka 2017 na 2018 umefanyika. Aidha, sura hii imehitimishwa kwa muhtasari wa uchambuzi katika stadi ya Kuhesabu.

### 4.2 Muundo wa Karatasi ya Upimaji wa Stadi ya Kuhesabu

Karatasi ya Upimaji wa utendaji wa wanafunzi katika Stadi ya Kuhesabu ilikuwa na maswali ishirini (20) yenye jumla ya alama 50 ambapo kila mwanafunzi alitakiwa kujibu maswali yote. Karatasi hii iliandaliwa kwa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wanaotumia lugha ya Kiswahili kujifunzia na lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wanaotumia Kiingereza kujifunzia.

Karatasi ya Stadi ya Kuhesabu ilipima umahiri wa wanafunzi kutambua namba zinazokosekana katika mpangilio wa namba (ngazi ya kwanza na pili), kujumlisha na kutoa (ngazi ya kwanza na ya pili) na kufumbua mafumbo. Kila umahiri katika maeneo haya ulipimwa kwa maswali matano. Maswali yaliyopima umahiri wa namba zinazokosekana, kujumlisha na kutoa yalipewa alama mbili kwa kila swali wakati yale yaliyopima umahiri wa kufumbua mafumbo yalipewa alama nne kila swali.

### 4.3 Vigezo vya Utendaji katika Stadi ya Kuhesabu

Upimaji wa utendaji wa wanafunzi kwa kila umahiri ulitumia vigezo vinne ambavyo ni utendaji hafifu kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali yasiyozidi mawili (2); utendaji wa wastani kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali matatu (3); utendaji mzuri kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali manne (4) na utendaji mzuri sana kwa mwanafunzi aliyejibu kwa usahihi maswali yote matano (5).

### 4.4 Utendaji wa Jumla Katika Stadi ya Kuhesabu

Takwimu za mahudhurio zinaonesha kuwa, wanafunzi 5,682 sawa na asilimia 81.9 walifanya upimaji katika Stadi ya Kuhesabu. Idadi ya wanafunzi wenye utendaji hafifu, wastani, mzuri na mzuri sana kwa kila umahiri uliopimwa umeoneshwa katika Jedwali Na.14.

**Jedwali Na. 14: Utendaji wa Jumla katika Stadi ya Kuhesabu**

| Umahiri Uliopimwa | Utendaji wa Wanafunzi | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hafifu | | Wastani | | Mzuri | | Mzuri sana | |
| | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % | Idadi | % |
| Kutambua Namba zinazokosekana | 2,098 | 36.92 | 1,176 | 20.70 | 953 | 16.77 | 1,455 | 25.61 |
| Kujumlisha | 1,800 | 31.68 | 1,117 | 19.66 | 1,427 | 25.11 | 1,338 | 23.55 |
| Kutoa | 2,646 | 46.57 | 1,404 | 24.71 | 1,025 | 18.04 | 607 | 10.68 |
| Kufumbua Mafumbo | 3,157 | 55.56 | 1,031 | 18.15 | 906 | 15.95 | 588 | 10.35 |


Jedwali Na.14 linaonesha kuwa asilimia 63.08, 68.32, 53.43 na 44.44 ya wanafunzi waliweza kujibu kwa usahihi maswali 3 hadi 5 katika dhana ya namba zinazokosekana, kujumlisha, kutoa na kufumbua mafumbo mtawalia. Hii inadhihirisha kwamba wanafunzi waliofanya upimaji walikuwa na utendaji unaoridhisha katika Stadi ya Kuhesabu.

## 4.5 Uchambuzi wa Majibu ya Wanafunzi

Uchambuzi wa kina ulifanyika ili kubaini utendaji wa wanafunzi kwa kila swali katika umahiri husika.


### 4.5.1 Umahiri wa Kutambua Namba Inayokosekana katika Mpangilio wa Namba

Umahiri wa kutambua namba inayokosekana katika mpangilio wa namba ulipimwa katika swali la 1 hadi 5. Maswali hayo yalilenga kupima uwezo wa mwanafunzi kubaini namba iliyokosekana na kuiandika katika nafasi iliyoachwa wazi kwa kila swali. Muhtasari wa utendaji wa wanafunzi katika swali la 1 hadi 5 umeoneshwa katika Chati Na.19.




**Chati Na. 19:** *Asilimia ya Wanafunzi waliojibu swali la 1 hadi 5 kwa usahihi.*

Chati Na. 19 inaonesha kuwa, wanafunzi wengi walijibu kwa usahihi swali la 1, 2 na 4 ukilinganisha na swali la 3 na 5. Hii inaonesha kwamba wanafunzi hao walikuwa na umahiri zaidi katika kuandika namba zinazokosekana katika mpangilio wa namba unaoachana kwa hatua moja na hatua kumi ukilinganisha na mpangilio wa namba unaoachana kwa hatua mbili na tano. Kielelezo Na. 24 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujaza namba inayokosekana kwenye mpangilio wa namba wenye achano la mbili na tano.




Andika namba inayokosekana katika nafasi iliyoachwa wazi.

1. 4, 5, 6, 7, 8, 9.
2. 15, 14, 13, 12, 11.
3. 44, 46, 46, 50, 52.
4. 70, 80, 90, 100.
5. 25, 30, 36, 40, 45.

**Kielelezo Na 24:** Majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali la 3 na *5.*


Pia, Chati Na. 19 inaonesha kuwa asilimia 82.88 waliweza kujibu swali la 1 kwa usahihi. Hivyo swali hili lilikuwa na kiwango kizuri zaidi cha utendaji. Aidha, asilimia 35.09 waliweza kujibu swali la 3 kwa usahihi hivyo swali hili lilikuwa na kiwango cha chini zaidi cha utendaji katika dhana ya kubaini namba zinazokosekana katika mpangilio wa namba. Hii inaonesha kuwa, wanafunzi walikuwa na umahiri zaidi katika kuhesabu namba zinazotofautiana kwa hatua mojamoja ikilinganishwa na kuhesabu namba ambazo zinatofautiana kwa hatua mbili mbili.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wanafunzi 732 sawa na asilimia 12.88 walishindwa kujibu kwa usahihi maswali yote 5. Baadhi walishindwa kubaini mahitaji ya swali na hivyo kutokuandika majibu. Wengine waliandika majibu ambayo hayana uhusiano na mfululizo wa namba zilizotolewa hivyo kuandika namba yoyote katika nafasi iliyoachwa wazi, jambo linaloonesha kuwa, hawakuwa na umahiri katika dhana iliyopimwa. Wanafunzi wengine hawakuzingatia nafasi ya mamoja na makumi katika uandishi wa namba. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliandika 53 badala ya 35 katika swali la 5. Kielelezo Na. 25 kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi ambao hawakujibu kwa usahihi maswali yote ambapo mwanafunzi mmoja aliandika namba zisizokuwa na uhusiano na mpangilio na mwingine alijumlisha au kutoa namba zilizoko kwenye mpangilio kimakosa ili kujaza namba inayokosekana.




**Kielelezo Na 25:** Wanafunzi waliokosa umahiri katika kujaza namba zinazokosekana kwenye mfuatano wa namba.

Hata hivyo, wanafunzi 1,455 sawa na asilimia 25.61 walijibu maswali yote matano kwa usahihi. Kwa mfano, katika swali la 1, waliweza kubaini kwamba namba zilizotolewa zinatofautiana kwa hatua moja na hivyo walijumlisha 5 na 1 na kupata 6 ambayo ni namba inayokosekana katika mfululizo huo. Vile vile, katika swali la 3, wanafunzi hao waliweza kuhesabu kwa hatua mbili mbili na kupata 48 ambayo ni namba iliyokuwa inafuata baada ya 46. Kielelezo Na. 26 kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi maswali yote matano.


Andika namba inayokosekana katika nafasi iliyoachwa wazi.

1. 4, 5, 6, 7, 8, 9.
2. 15, 14, 13, 12, 11.
3. 44, 46, 48, 50, 52.
4. 70, 80, 90, 100.
5. 25, 30, 35, 40, 45.

Write the missing number:

1. 4, 5, 6, 7, 8, 9.
2. 15, 14, 13, 12, 11.
3. 44, 46, 48, 50, 52.
4. 70, 80, 90, 100.
5. 25, 30, 35, 40, 45.


**Kielelezo Na 26:** Majibu ya wanafunzi waliojaza kwa usahihi namba zinazokosekana katika swali la 1 hadi 5.

### 4.5.2 Umahiri wa Kujumlisha

Umahiri wa wanafunzi katika kujumlisha namba zenye tarakimu zisizozidi tatu ulipimwa katika swali la 6 hadi 10 katika dhana tano kama ifuatavyo:


(a) Kujumlisha namba mbili zenye tarakimu moja;
(b) Kujumlisha namba yenye tarakimu mbili kwa namba yenye tarakimu moja bila kubeba;
(c) Kujumlisha namba yenye tarakimu mbili kwa namba yenye tarakimu moja kwa kubeba mara moja;
(d) Kujumlisha namba mbili zenye tarakimu mbili kila moja kwa kubeba mara moja na
(e) Kujumlisha fedha.

Uchambuzi wa takwimu za utendaji katika umahiri wa kujumlisha namba unaonesha kuwa asilimia 68.36 ya wanafunzi waliofanya upimaji walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Miongoni mwao wanafunzi 1,338 sawa na asilimia 23.55 walijibu maswali yote matano kwa usahihi. Wanafunzi hao walipanga kazi zao vizuri na kuandika majibu sahihi kwenye nafasi iliyoachwa wazi, jambo linaloonesha kuwa walikuwa na umahiri mzuri sana. Kielelezo Na. 27 ni sampuli ya majibu ya wanafunzi waliojibu maswali yote matano kwa usahihi.




**Kielelezo Na 27:** Majibu ya wanafunzi waliojumlisha namba walizopewa kwa usahihi katika swali la 6 hadi 10.

Uchambuzi zaidi wenye lengo la kubaini asilimia ya wanafunzi waliojibu kila swali kwa usahihi lililopima umahiri wa kujumlisha namba ulifanyika. Matokeo ya uchambuzi yamewasilishwa katika Chati Na. 20.





**Chati Na. 20:** *Wanafunzi Waliojibu Swali la 6 hadi 10 kwa Usahihi.*

Chati Na. 20 inaonesha kuwa wanafunzi wengi (89.63%) walikuwa na utendaji mzuri zaidi katika kujumlisha namba mbili zenye tarakimu moja katika swali la 6 na wanafunzi 4,288 sawa na asilimia 75.47 walikuwa na utendaji mzuri katika kujumlisha namba yenye tarakimu mbili na namba yenye tarakimu moja bila kubeba katika swali la 7.

Hata hivyo, umahiri wa wanafunzi ulipungua katika kujumlisha namba zilizohitaji kubeba kutoka mamoja kwenda makumi (ngazi ya pili). Kwa mfano, katika swali la 8 ambalo lilihusu $28+6=$, baadhi ya wanafunzi waliandika 24 au 214 na wengine waliandika 43 badala ya 34. Pia, katika swali la 9 ambalo lilihusu $47+16=$, baadhi ya wanafunzi waliandika 513 au 53 na wengine 36 badala 63. Hii inaonesha kuwa, baadhi ya wanafunzi hao hawakuwa na umahiri wa kubeba moja iliyotokana na kujumlisha namba zilizopo kwenye mamoja ili kwenda kuijumlishia kwenye namba zilizopo kwenye nafasi ya makumi na wengine hawakuzingatia utaratibu wa uandishi wa namba katika nafasi ya makumi na mamoja.

Aidha, wanafunzi 3,257 sawa na asilimia 57.32 walishindwa kujibu kwa usahihi swali la 10 lililohusu kujumlisha fedha na hivyo swali hili lilikuwa na utendaji wa chini zaidi ukilinganisha na maswali mengine yaliyopima kujumlisha. Hii ni kutokana na kutokupanga vizuri namba walizopewa kwa usahihi katika mamoja, makumi na mamia kabla ya kujumlisha fedha hizo. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi walijumlisha mamia kwa makumi na makumi kwa mamoja na kuishia kupata 900 na wengine waliunganisha namba walizopewa kupata 40,050 badala ya kuzijumlisha ili kupata 450. Kielelezo Na. 28 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi.


Tafuta Majibu:

6. 1 + 7 = 8

7. 12 + 5 = 17


8. 28 + 6 = 24

9. 47 + 16 = 513

10. Shilingi 400 + shilingi 50 = 900

**Kielelezo Na 28:** Mwanafunzi aliyeshidwa kujibu kwa usahihi swali la 8, 9 na 10.

Uchambuzi zaidi unaonesha kwamba wanafunzi 431 sawa na asilimia 7.58 walishindwa kujibu kwa usahihi maswali yote matano. Kielelezo Na. 29 ni sampuli ya majibu ya wanafunzi wenye utendaji hafifu katika kujumlisha namba.




**Kielelezo Na 29:** Majibu ya wanafunzi walioshindwa kujibu kwa usahihi swali la 6 hadi 10 hivyo kuonekana kukosa umahiri katika dhana zilizopimwa.

### 4.5.3 Umahiri wa Kutoa

Swali la 11 - 15 yalipima umahiri wa wanafunzi kutoa namba. Maswali hayo yalipima uwezo wa wanafunzi katika:

(a) Kutoa namba mbili zenye tarakimu moja;


(b) Kutoa namba mbili, moja yenye tarakimu mbili na nyingine yenye tarakimu moja bila kuchukua;

(c) Kutoa namba mbili, moja yenye tarakimu mbili na nyingine yenye tarakimu moja kwa kuchukua;

(d) Kutoa namba mbili zenye tarakimu mbili kwa kuchukua;

(e) Kutoa fedha zenye tarakimu tatu kwa kuchukua mara moja.


Uchambuzi wa takwimu za utendaji ulifanywa ili kubaini asilimia ya wanafunzi waliomudu kila swali. Chati Na. 21 inaonesha matokeo ya uchambuzi huo.




**Chati Na. 21:** *Asilimia ya wanafunzi waliojibu swali la 11 hadi 15 kwa usahihi.*


Chati Na. 21 inaonesha kuwa, swali la 11 liliongoza kwa kufanyika vizuri likifuatiwa na swali la 12. Asilimia 75.82 waliweza kutoa kwa usahihi namba mbili zenye tarakimu moja katika swali la 11. Pia, asilimia 64.20 waliweza kutoa kwa usahihi namba mbili, moja yenye tarakimu mbili na nyingine yenye tarakimu moja bila kuchukua katika swali la 12.

Pia, Chati Na. 21 inaonesha kuwa umahiri wa wanafunzi katika kutoa namba zinazohitaji dhana ya kuchukua uliopimwa katika swali la 13, 14 na 15 ulikuwa ni asilimia 54.38, 31.19 na 21.52 mtawalia. Hii inaonesha kuwa umahiri wa wanafunzi ulipungua katika maswali ya kutoa kwa kuchukua (ngazi ya pili) na ulipungua kadri idadi ya tarakimu ilivyoongezeka. Kielelezo Na. 30 kinaonesha sampuli ya majibu ya wanafunzi hao.




**Kielelezo Na. 30:** *Majibu ya wanafunzi waliojibu kwa usahihi swali la 11 na 12 na kushindwa swali la 13, 14 na 15.*

Aidha, asilimia 16.47 ya wanafunzi waliofanya upimaji huu walishindwa kujibu kwa usahihi maswali yote 5 yaliyopima umahiri wa kutoa kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 31.




**Kielelezo Na 31:** Majibu ya wanafunzi walioshindwa maswali yote yaliyopima dhana ya kutoa.

Matokeo ya upimaji uliofanywa mwaka 2017 pia yanaonesha kuwa dhana ya kutoa kwa kuchukua na hesabu za fedha iliwatatiza wanafunzi walio wengi.

Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa, sababu zilizochangia wanafunzi kukosa maswali yote ni pamoja na:


(a) Kukosa umahiri katika Kuhesabu, Kusoma na Kuandika namba zisizozidi tarakimu tatu, hivyo kuandika majibu yasiyoeleweka.

(b) Kunakili maswali yaliyotolewa bila kuandika majibu au kuandika majibu yasiyo sahihi.

(c) Kutokubaini kama walikopa namba ama katika nafasi ya makumi katika swali la 13 na 14 au katika nafasi ya mamia katika swali la 15 wakati wa kutoa namba zilizotolewa.

(d) Kushindwa kutofautisha dhana ya kutoa na kujumlisha.


Kwa upande mwingine, uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa asilimia 10.68 ya wanafunzi waliofanya upimaji huu walijibu kwa usahihi maswali yote matano yaliyopima umahiri wa kutoa kama inavyojidhihirisha katika sampuli za majibu katika Kielelezo Na. 32.




**Kielelezo Na 32:** *Majibu ya wanafunzi waliojibu swali la 11 hadi 15 kwa usahihi na hivyo kuonekana kuwa na umahiri wa kujumlisha ngazi ya kwanza na ya pili.*

### 4.5.4 Umahiri wa Kufumbua Mafumbo

Swali la 16 hadi 20 yalipima umahiri wa wanafunzi kufumbua mafumbo yanayohusiana na matumizi ya dhana ya kujumlisha na kutoa katika maisha yao ya kila siku. Utendaji wa wanafunzi umeoneshwa katika Chati Na. 22.




**Chati Na. 22:** *Asilimia ya wanafunzi waliojibu swali la 16 hadi 20 kwa usahihi.*

Chati Na. 22 inaonesha kuwa swali la 16 ndilo lililoongoza kwa kufanyika vizuri likifuatia swali la 19, 17 na 18. Swali la 20 lilikuwa na kiwango cha chini zaidi cha utendaji katika maswali ya mafumbo.

Katika maswali ya mafumbo asilimia 44.44 walikuwa na utendaji wa wastani, mzuri na mzuri sana. Miongoni mwao asilimia 10.35 walikuwa na utendaji mzuri sana kwani waliweza kujibu maswali yote

matano kwa usahihi. Wanafunzi hawa waliweza kutumia matendo ya kujumlisha na kutoa kwa usahihi na walipanga kazi zao kwa mwandiko mzuri kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 33.

16. Mary ana machungwa 240 na kaka yake ana machungwa 342. Je, jumla wana machungwa mangapi?

$$\begin{array}{r} 240 \\ +\ 342 \\ \hline 582 \end{array}$$

jumla ana machungwa 582

17. Sara alikuwa na pipi 450. Alimgawia rafiki yake pipi 220. Je, alibakiwa na pipi ngapi?


$$\begin{array}{r} 450 \\ -\ 220 \\ \hline 230 \end{array}$$

alibakiwa na pipi 230

18. Darasa la pili lina wasichana 70 na wavulana 90. Je, darasa hilo lina wanafunzi wangapi?

$$\begin{array}{r} 70 \\ +\ 90 \\ \hline 160 \end{array}$$

jumla darasa lina wanafunzi 160


19. Juma alinunua kalamu kwa shilingi 150 na daftari kwa shilingi 500. Je, alilipa shilingi ngapi?

150
+ 500
650

jumla ni shilingi 650

20. Musa alipewa shilingi 600 na baba yake. Alitumia shilingi 250. Je, alibakiwa na shilingi ngapi?

600
− 250
350

alibakiwa na shilingi 350

**Kielelezo Na 33:** Majibu ya mwanafunzi aliyejibu swali la 16 hadi 20 kwa usahihi.


Kwa upande mwingine, zaidi ya nusu ya wanafunzi (55.54%) walikuwa na utendaji hafifu na miongoni mwao asilimia 26.59 walishindwa maswali yote. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi unaonesha kuwa sababu zilizochangia wanafunzi kuwa na utendaji hafifu ni pamoja na:

(a) Wanafunzi kushindwa kutumia kwa usahihi matendo ya kujumlisha au kutoa. Kwa mfano, katika swali la 16, 18 na 19 baadhi ya wanafunzi walitoa badala ya kujumlisha namba walizopewa. Hali kadhalika, katika swali la 17 na 20 wanafunzi wengine walijumlisha badala ya kutoa namba zilizotolewa. Jambo hili linaloonesha kuwa walishindwa kuelewa maana ya maneno “alibakiwa na”, “jumla” yaliyotumika katika maswali.

(b) Wanafunzi kunakili maswali yaliyotolewa badala ya kukokotoa majibu; kutojibu maswali na wengine kuandika majibu yasiyoeleweka.

(c) Wanafunzi kufanya makosa wakati wa kujumlisha au kutoa, hali iliyosababisha kupata majibu yasiyo sahihi.

Kielelezo Na. 34 na 35 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi maswali yote matano ya mafumbo.


16. Mary ana machungwa 240 na kaka yake ana machungwa 342. Je, jumla wana machungwa mangapi?

Mary anamachungwa 240 naka kayakeanamachungwa

342 Je jumla Wanamachungwa mangapi?

machungwa 240

machungwa - 342 = 102

17. Sara alikuwa na pipi 450. Alimgawia rafiki yake pipi 220. Je, alibakiwa na pipi ngapi?


Sara alikua napipi 450 Alimgawia rafiki yake pipi 220
Je, alibakiwanapipingapi? 450
+ 220
630

18. Darasa la pili lina wasichana 70 na wavulana 90. Je, darasa hilo lina wanafunzi wangapi?

Darasa la pili lina wasichana 70 na wavulana 90 Je,
darasa hilo lina wanafunzi wangapi? 70
+ 90
170

19. Juma alinunua kalamu kwa shilingi 150 na daftari kwa shilingi 500. Je, alilipa shilingi ngapi?

Juma alinunua kalamu kwa shilingi 150 na dafta
ri kwa shilingi 500 Je, alilipa shilingi ngapi?
150
− 500
050




20. Musa alipewa shilingi 600 na baba yake. Alitumia shilingi 250. Je, alibakiwa na shilingi ngapi?

Musa alipewa shilingi 600 na baba yake Alitumia shilingi 250 Je, alibakiwa na shilingi ngapi?

$$\begin{array}{r} 600 \\ -250 \\ \hline 450 \end{array}$$

**Kielelezo Na 34:** Mwanafunzi aliyetumia matendo ya kutoa na kujumlisha kimakosa katika swali la 16, 17 na 19. Katika swali la 18 na 20 alitumia matendo sahihi lakini alikosea katika kujumlisha au kutoa namba zilizotolewa.



17. Sara alikuwa na pipi 450. Alimgawia rafiki yake pipi 220. Je, alibakiwa na pipi ngapi?

18. Darasa la pili lina wasichana 70 na wavulana 90. Je, darasa hilo lina wanafunzi wangapi?

**Kielelezo Na 35:** Sampuli ya majibu mwanafunzi yasiyoeleweka.


## 4.6 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia, Mahali Shule ilipo, Jinsi na Shule Zilizofanya Upimaji Mwaka 2017 na 2018 na Shule 33 Zilizopimwa Mwaka 2017 na 2018

Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi ulifanyika kati ya shule zinazotumia lugha ya Kiswahili kufundishia na zile zinazotumia lugha ya Kiingereza kufundishia; shule za mjini na vijijini; wanafunzi wavulana na wasichana na shule zilizofanya upimaji mwaka 2017 na 2018.

Lengo la kufanya ulinganifu ni kubaini kama kuna tofauti ya utendaji wa wanafunzi katika makundi hayo ili kuweza kutoa mapendekezo kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

### 4.6.1 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia

Takwimu za usajili zinaonesha kuwa, wanafunzi 4,760 walifanya upimaji katika shule zinazotumia lugha ya Kiswahili na wanafunzi 922 katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza. Muhtasari wa taarifa ya ulinganifu umeoneshwa katika Chati Na.23.





**Chati Na. 23:** *Ulinganifu wa Utendaji kwa Kuzingatia Lugha ya Kufundishia.*

Chati Na. 23 inaonesha kuwa, asilimia 73.45 ya wanafunzi waliofanya upimaji walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana katika shule zinazotumia lugha ya Kiswahili. Katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza asilimia 98.37 ya wanafunzi walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana.

Hivyo, wanafunzi kutoka shule zinazotumia lugha ya Kiingereza walikuwa na kiwango kizuri zaidi cha utendaji kwa asilimia 24.92 ikilinganishwa na wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiswahili kufundishia. Matokeo haya hayatofautiani sana na matokeo ya upimaji uliofanyika mwaka 2017 ambapo wanafunzi wanaosoma katika shule zinazotumia lugha ya Kiingereza walikuwa na kiwango kizuri zaidi cha utendaji kwa asilimia 25.09.

### 4.6.2 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Shule za Mijini na Vijijini

Upimaji wa Stadi ya Kuhesabu ulihusisha wanafunzi 4,080 kutoka shule za mijini na 1,602 kutoka shule za vijijini. Ulinganifu wa utendaji umefanyika ili kubaini kama kuna tofauti ya utendaji kati ya wanafunzi wa mijini na vijijini. Matokeo ya ulinganifu huu yameoneshwa katika Chati Na. 24.





**Chati Na. 24:** *Ulinganifu wa Utendaji kwa Shule za Mijini na Vijijini*

Chati Na. 24 inaonesha kuwa, wanafunzi wenye utendaji wa wastani hadi mzuri sana kwa shule za mijini ni asilimia 80.78 na kwa shule za vijijini ni asilimia 69.10. Hii inaonesha kuwa, wanafunzi wanaotoka shule za mijini wana utendaji mzuri zaidi ikilinginishwa na wanafunzi wanaotoka shule za vijijini. Matokeo haya yametofautiana na matokeo ya upimaji uliofanyika mwaka 2017 ambapo asilimia 79.49 ya wanafunzi kutoka shule za vijijini walikuwa na utendaji mzuri zaidi ukilinganisha na asilimia 75.33 ya wanafunzi kutoka shule za mijini.

### 4.6.3 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi kwa Kuzingatia Jinsi

Jumla ya wanafunzi 5,682 walifanya Upimaji katika Stadi ya Kuhesabu ambapo wanafunzi 2,819 walikuwa wavulana na 2,863 walikuwa wasichana. Chati Na. 25 inaonesha muhtasari wa matokeo ya ulinganifu katika utendaji.





**Chati Na. 25:** *Ulinganifu wa Utendaji kwa kuzingatia jinsi.*

Chati Na. 25 inaonesha kuwa, asilimia 77.51 ya wavulana walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana wakati wasichana walikuwa asilimia 77.47. Hii inaonesha kuwa wavulana walikuwa na kiwango cha utendaji kizuri zaidi kwa asilimia 0.04.

### 4.6.4 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Shule 33 Zilizopimwa Mwaka 2017 na Kupimwa Tena 2018

Takwimu za usajili zinaonesha kuwa, shule 33 zilizopimwa kwa mara ya pili mwaka 2018 zilikuwa na jumla ya wanafunzi 3,086 wakati mwaka 2017 zilikuwa na wanafunzi 2,989. Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi katika shule hizo kwa mwaka 2017 na 2018 umefanyika na matokeo yameoneshwa katika Chati Na. 26.





**Chati Na. 26:** *Ulinganifu wa Utendaji kwa Shule zilizopimwa 2017 na kupimwa kwa mara nyingine mwaka 2018.*

Chati Na. 26 inaonesha kuwa, wanafunzi waliokuwa na utendaji wa wastani, mzuri na mzuri sana, mwaka 2017 walikuwa asilimia 79.83 wakati mwaka 2018 walikuwa asilimia 74.69. Hivyo, utendaji wa shule hizo mwaka 2018 umeshuka kwa asilimia 5.14 ukilinganishwa na mwaka 2017.

### 4.6.5 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi katika Shule 33 Zilizopimwa kwa Mara ya Kwanza na Mara Pili Mwaka 2018

Jumla ya wanafunzi katika shule 33 zilizofanyiwa upimaji kwa mara ya pili ilikuwa 3,086 na jumla ya wanafunzi katika shule 33 zilizofanyiwa upimaji kwa mara ya kwanza ilikuwa 2,589 mwaka 2018. Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi katika makundi haya mawili umeoneshwa katika Chati Na. 27.





**Chati Na. 27:** *Ulinganifu wa Utendaji kwa Shule zilizopimwa kwa mara ya kwanza na shule zilizopimwa mara ya pili.*

Chati Na. 27 inaonesha kuwa asilimia 74.69 ya wanafunzi katika shule 33 zilizofanya upimaji kwa mara ya pili walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Chati hii inaonesha pia, asilimia 80.82 ya wanafunzi katika shule 33 zilizofanya upimaji kwa mara ya kwanza walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Hii inaonesha kuwa, wanafunzi katika shule 33 zilizopimwa kwa mara ya kwanza wana kiwango kizuri zaidi cha utendaji ikilinganishwa na wanafunzi katika shule 33 zilizopimwa kwa mara nyingine 2018.

### 4.6.6 Ulinganifu wa Utendaji wa Wanafunzi mwaka 2017 na 2018

Idadi ya wanafunzi katika shule zilizofanyiwa upimaji mwaka 2018 ilikuwa 5,682 na mwaka 2017 ilikuwa 6,195. Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa miaka hiyo miwili umeoneshwa katika Chati Na. 28.




**Chati Na. 28:** *Ulinganifu wa utendaji wa wanafunzi kwa Shule 66 zilizofanya upimaji 2017 na 2018.*

Chati Na. 28 inaonesha kuwa asilimia 77.49 ya wanafunzi waliofanya upimaji mwaka 2018 walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana wakati mwaka 2017 ulikuwa asilimia 76.95. Hii inaonesha kwamba kiwango cha utendaji kimeongezeka kwa asilimia 0.54.

## 4.6 Muhtasari wa Uchambuzi Katika Stadi ya Kuhesabu

Katika maswali yaliyopima umahiri wa namba zinazokosekana, wanafunzi walionesha kuwa na utendaji mzuri katika kukamilisha mpangilio wa namba unaoongezeka au kupungua kwa hatua 1 na 10. Aidha, mpangilio unaoongezeka kwa hatua mbili na tano ulionekana kuwatatiza wanafunzi wengi.

Katika maswali yaliyopima umahiri wa kujumlisha, wanafunzi walionesha kuwa na utendaji mzuri katika kujumlisha namba mbili zenye tarakimu moja na kujumlisha namba yenye tarakimu mbili na namba yenye tarakimu moja bila kubeba. Hata hivyo, wanafunzi wengi walionesha kushindwa kujumlisha kwa usahihi namba zenye tarakimu mbili na namba zenye tarakimu tatu hususan kama ujumlishaji ulihitaji kutumia dhana ya kubeba.

Katika maswali yaliyopima umahiri wa kutoa, wanafunzi wengi walionesha kuwa na utendaji mzuri katika kutoa namba mbili zenye tarakimu moja na kutoa namba yenye tarakimu moja toka kwenye namba yenye tarakimu mbili bila kukopa. Aidha, wanafunzi wengi walishindwa kujibu kwa usahihi maswali yaliyohitaji dhana ya kukopa.

Katika maswali ya mafumbo, karibia nusu ya wanafunzi waliofanya upimaji walishindwa kukokotoa majibu sahihi. Hii ilitokana na sababu mbalimbali kama vile wanafunzi kushindwa kubaini mahitaji ya swali, wanafunzi kufanya makosa wakati wa kujumlisha au kutoa na wanafunzi kunakili maswali yaliyotolewa badala ya kukokotoa majibu, kutojibu maswali na wengine kuandika majibu yasiyoeleweka.

# SURA YA TANO

## UCHAMBUZI WA TAARIFA ZA USIMAMIZI

### 5.1 Uchambuzi wa Taarifa za Shule

Baraza la Mitihani liliandaa dodoso kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali zilizotumika wakati wa upimaji na kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK zitakazowezesha kutoa maoni yenye kuboresha changamoto zinazoendelea kujitokeza. Dodoso hizo zililenga kubaini hali ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK ili kuweza kutoa ushauri kwa lengo la kuboresha kiwango cha elimu inayotolewa katika ngazi hiyo.

Katika kupata taarifa husika, aina mbili za dodoso zilitumika: moja iliyokamilishwa na walimu wakuu 66 na nyingine wasimamizi 696 waliosimamia upimaji wa stadi za KKK. Taarifa zilizohitajika katika dodoso hizo ni pamoja na ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi, mahudhurio ya wanafunzi katika kila stadi, ujuzi wa walimu katika kufundisha stadi za KKK na uwepo wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Taarifa nyingine ni hali ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wa Darasa la I na la II kwa mwaka 2018.

#### 5.1.1 Taarifa za Shule kwa Ujumla

Dodoso la Mwalimu Mkuu lililenga kupata taarifa kuhusu uwepo wa mihtasari ya ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK. Lengo lilikuwa kubaini ikiwa ufundishaji na ujifunzaji unazingatia taratibu kama zilivyoainishwa katika mtaala wa elimumsingi.

Uchambuzi wa majibu ya dodoso umebainisha kuwa, shule zote 66 zilizohusika katika upimaji wa mwaka 2018 sawa na asilimia 100, zilikuwa na mihtasari ya kufundishia Stadi za KKK kwa Darasa la Kwanza na la Pili ikilinganishwa na asilimia 98.2 ya mwaka 2017. Takwimu hizi zinaonesha kuwa juhudi za makusudi zilifanyika kuwezesha shule zote zilizohusika katika upimaji wa mwaka 2018 kuwa na mihtasari ya kufundishia Stadi za KKK.

Taarifa nyingine zilizohitajika kutoka kwa walimu wakuu ni idadi ya mikondo na wanafunzi katika kila mkondo. Umuhimu wa taarifa hii ilikuwa kuona idadi ya ukomo ya wanafunzi 40 kwa mkondo kama iliyoelekezwa katika Mtaala wa Elimu ya Msingi Tanzania 2007

inazingatiwa. Majibu ya Walimu Wakuu yameoneshwa katika Jedwali Na.15.

**Jedwali Na. 15: Idadi ya Wanafunzi katika Mkondo**

| Na. | Mfiko wa Idadi ya Wanafunzi | Idadi ya Shule Darasa la I | | Idadi ya Shule Darasa la II | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Idadi | % | Idadi | % |
| 1. | 09-40 | 42 | 63.6 | 41 | 62.1 |
| 2. | 41 - 50 | 5 | 7.6 | 3 | 4.5 |
| 3. | 51 - 60 | 4 | 6 | 4 | 6 |
| 4. | 61 - 70 | 1 | 1.5 | 2 | 3 |
| 5. | 71 - 80 | 3 | 4.5 | 6 | 9.1 |
| 6. | 81 - 90 | 2 | 3 | 1 | 1.5 |
| 7. | 91- 100 | 4 | 6 | 1 | 1.5 |
| 8. | 101+ | 5 | 7.6 | 8 | 12.1 |

**N= 66**

Jedwali Na.15 linaonesha kuwa, shule 42 sawa na asilimia 63.6 zilikuwa na mikondo yenye idadi ya wanafunzi kwa ukomo ulioelekezwa katika darasa la I na shule 41 sawa na asilimia 62.1 zilikuwa na idadi hiyo kwa darasa la II. Takwimu hizo zinaonesha kuwa, idadi kubwa ya shule za msingi zilizohusika katika upimaji wa stadi za KKK 2018 hazikuwa na msongamano mkubwa wa wanafunzi katika vyumba vya madarasa. Kwa takwimu hizo, shule 25 sawa na asilimia 37.9 zilikuwa na mikondo yenye wanafunzi zaidi ya idadi inayokubalika kwa darasa la II na shule 24 sawa na asilimia 36.9 kwa darasa la I. Kati ya shule zilizokuwa na msongamano wa wanafunzi darasani, nane, sawa na asilimia 12.1 kwa darasa la II na 5 (7.6%) darasa la I zilikuwa na mikondo yenye wanafunzi zaidi ya 100.

Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa, kwa shule zinazotumia mfumo wa lugha ya kiingereza shule moja ilikuwa na mikondo yenye wanafunzi zaidi ya 40 kwa darasa la I. Uchambuzi zaidi wa madodoso unaonesha kuwa, sababu za baadhi ya shule kuwa na mikondo yenye idadi kubwa ya wanafunzi ni uchache wa vyumba vya madarasa na uhaba wa walimu wanaofundisha stadi za KKK.

Takwimu hizi zinaonesha kuwa, bado kuna changamoto ya msongamano wa wanafunzi wa darasa la I na la II, hivyo juhudi za makusudi zinahitajika kuondoa changamoto hiyo.

### 5.1.2 Ufundishaji wa Wanafunzi na Mafunzo kwa Walimu wa Stadi za KKK

Dodoso la Mwalimu Mkuu lililenga pia kupata taarifa za ufundishaji na mafunzo kwa walimu wa stadi za KKK. Takwimu zinaonesha kuwa, shule zote 66 sawa na asilimia 100 zilizofanya upimaji zilikuwa na angalau mwalimu mmoja anayefundisha katika darasa la I na II. Hata hivyo, taarifa hizo zinaonesha kuwa kati ya walimu 178 wanaofundisha Stadi za KKK katika shule hizo, walimu 71 sawa na asilimia 39.89 walikuwa wamepata mafunzo maalum kwa ajili ya ufundishaji wa stadi husika.

Takwimu pia zinaonesha kuwa, asilimia ya walimu wenye mafunzo ya KKK walioshiriki katika upimaji wa mwaka 2018 imepungua sana ikilinganishwa na asilimia 81.9 katika upimaji wa mwaka 2017. Upungufu huo ulitokana na upimaji wa mwaka 2018 kuhusisha walimu wa madarasa ya juu (III na VII) wakati mwaka 2017 ulihusisha walimu wa madarasa ya I na II tu.

### 5.1.3 Hali ya Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Walimu wakuu waliulizwa kuhusu upatikanaji wa vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia kama vile vitabu vya kiada, ziada na vifaa vingine vinavyotumika kufundishia kila Stadi. Majibu ya walimu hao yameainishwa katika Jedwali Na.16.

**Jedwali Na. 16: Upatikanaji wa Vitabu na Vifaa vya Kujifunzia KKK**

| Na. | Swali | Idadi ya waliojibu | Idadi | % |
|---|---|---|---|---|
| (a) | Upatikanaji wa Vitabu vya kiada vya kufundishia Stadi za Kuhesabu | 66 | 62 | 93.9 |
| (b) | Upatikanaji wa vitabu vya ziada vya mazoezi ya Stadi ya Kuhesabu | 66 | 57 | 86.4 |
| (c) | Uwepo wa Vifaa vya kufundishia Stadi ya Kuhesabu, kama vile vihesabio | 66 | 61 | 92.4 |
| (d) | Uwepo wa vitabu vya kiada na Vifaa vya kufundishia Stadi ya Kuandika | 66 | 56 | 87.9 |
| (e) | Uwepo wa vitabu vya kiada vya | 66 | 61 | 92.4 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | kufundishia Stadi ya Kusoma | | | |
| (f) | Upatikanaji wa vifaa vinavyolenga kuendeleza Stadi ya Kusoma | 66 | 59 | 89.4 |
| (g) | Uwepo wa vitabu vya kiada vya kufundishia Stadi ya Kuandika | 66 | 61 | 92.4 |

Jedwali Na. 16 linaonesha kuwa, upatikanaji wa vitabu vya kufundishia stadi zote katika shule zilizoteuliwa ulikuwa mzuri. Upatikanaji wa vitabu vya kiada vya Stadi ya Kuhesabu ulikuwa mzuri zaidi kwa kuwa na asilimia 93.9, Stadi ya Kuandika asilimia 92.4 na vitabu kwa ajili ya Stadi ya Kusoma asilimia 92.4. Pia, uwepo wa vitabu vya ziada kwa ajili ya kufundishia Stadi ya Kuhesabu ulikuwa mzuri kwa asilimia 86.4 na vifaa vingine kwa ajili ya kukuzia umahiri wa somo hilo ulikuwa mzuri kwa asilimia 92.4. Kwa upande mwingine, upatikanaji wa vifaa kama vile vitabu vya hadithi za watoto wadogo kwa ajili kukuzia Stadi ya Kusoma ulikuwa mzuri (89.4%).

Takwimu hizo zinaonesha kuwa, upatikanaji wa vitabu vya kiada ulikuwa mzuri zaidi kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na mwaka 2017. Kwa mfano, mwaka 2017 upatikanaji wa vitabu vya kiada vya kufundishia Stadi ya Kuhesabu ulikuwa asilimia 93.3 wakati mwaka 2018 ulikuwa asilimia 93.9. Aidha, upatikanaji wa vitabu vya ziada vya maozezi kwa Stadi hiyo uliongezeka kutoka asilimia 85.0 mwaka 2017 hadi asilimia 86.4 mwaka 2018. Kwa upande mwingine, upatikanaji wa vifaa vya kufundishia stadi hiyo uliongezeka kutoka asilimia 91.8 mwaka 2017 hadi asilimia 92.4 mwaka 2018.

Uwepo wa zana za kufundishia na kujifunzia pamoja na kuongezeka kwa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kunaonesha kuwa, juhudi kubwa za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za KKK zimefanywa na Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), uongozi wa elimu ngazi ya Mikoa, Wilaya hadi Shule.

### 5.1.4 Miundombinu na Mazingira ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Ili kupata taarifa kuhusu hali halisi ya mazingira ya ufundishaji walimu wakuu walitakiwa kutoa taarifa kuhusu uwepo wa madawati, meza na viti vya kukalia wanafunzi na walimu wanaofundisha stadi za KKK. Pia waliulizwa kuhusu uwepo wa vyumba vya madarasa na upatikanaji wa chumba maalum kinachotumika kama maktaba kwa ajili ya wanafunzi

na walimu kujisomea wawapo shuleni. Muhtasari wa majibu ya walimu ni kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 17.

**Jedwali Na. 17: Muhtasari wa Majibu ya Walimu Kuhusu Mazingira ya Kujifunzia KKK**

| Na. | Swali | Idadi ya waliojibu | Idadi | % |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Uwepo wa madawati, meza na viti vya kukalia wanafunzi na walimu wa Darasa la I na la II shuleni. | 66 | 56 | 84.8 |
| 2. | Hali ya uwepo wa vyumba vya madarasa ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi wa Darasa la I na la II waliopo shuleni. | 66 | 52 | 78.8 |
| 3. | Upatikanaji wa chumba maalum au maktaba ambapo watoto na walimu wanaweza kuazima vitabu ili kuwawezesha wanafunzi kujifunza zaidi stadi za KKK hata baada ya muda wa shule ukoje? | 66 | 36 | 54.5 |

Kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 17, asilimia 78.8 ya walimu waliripoti kuwepo kwa vyumba vya kutosha vya madarasa na uwepo wa samani kama vile madawati, viti na meza kwa kiwango cha asilimia 84.8. Takwimu hizo zinaonesha uwepo wa ongezeko dogo la samani ikilinganishwa na la mwaka 2017 ambapo zilikuwa zinapatikana kwa asilimia 84.6. Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa shule ambazo zilikuwa na maktaba au chumba maalum kwa ajili ya watoto na walimu kuweza kuazima vitabu na kuwawezesha wanafunzi kujisomea zaidi baada ya muda wa shule ni asilimia 54.5.

### 5.1.5 Mahudhurio ya Wanafunzi

Taarifa ya mahudhurio ya wanafunzi katika dodoso la wasimamizi zinaonesha kuwa, wanafunzi waliofanya upimaji ni 5,771 (82.04%) na idadi ya wanafunzi ambao hawakufanya upimaji kwa sababu mbalimbali ni 1,263 (17.96%). Baadhi ya sababu zilizobainishwa na wasimamizi zimeoneshwa katika Jedwali Na .18.

**Jedwali Na. 18: Taarifa za Wanafunzi Wasiofanya Upimaji**

| Na | Sababu | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1. | Utoro | 867 | 68.6 |
| 2. | Kuhama shule | 198 | 15.7 |
| 3. | Kukariri (Kurudia) darasa | 61 | 4.8 |
| 4. | Ugonjwa | 25 | 2.1 |
| 5. | Kufariki | 07 | 0.6 |
| 6. | Hakuna sababu iliyotolewa | 105 | 8.6 |
| | **Jumla** | **1263** | **100** |

**N= 1,263**

Jedwali Na. 18 linaonesha kuwa, utoro ulikuwa ni sababu kubwa iliyoathiri mahudhurio ya wanafunzi katika upimaji ambapo ulikuwa asilimia 68.6. Sababu nyingine ilikuwa ni wanafunzi kuhama shule iliyokuwa na asilimia 15.7, na asilimia 4.8 walikariri darasa la pili. Baadhi ya wanafunzi (2.1) hawakujitokeza kwa sababu ya ugonjwa na 0.6 walifariki dunia. Aidha, baadhi ya wasimamizi walikiri kuwepo kwa wanafunzi ambao hawakufanya upimaji (8.6%) bila kubainisha sababu ya kutohudhuria kwao.

Idadi ya wanafunzi watoro katika upimaji wa mwaka 2018 imepungua kwa asilimia 17.9 ikilinganishwa na asilimia 86.5 ya watoro katika upimaji wa mwaka 2017. Mafanikio hayo yanaonesha kuwa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknoloji pamoja na Wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) zilishirikiana vizuri na uongozi wa elimu ngazi ya Mikoa, Wilaya hadi ngazi ya shule pamoja na wazazi katika kutatua changamoto hii.

# SURA YA SITA

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 6.1 Hitimisho

Kwa ujumla utendaji wa wanafunzi katika stadi zote (Kusoma, Kuandika na Kuhesabu) umeongezeka ukilinganishwa na Upimaji wa mwaka 2017. Katika stadi ya Kusoma, wanafunzi wengi (90.22%) walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Hata hivyo, asilimia 9.78 ya wanafunzi walikuwa na utendaji hafifu. Wanafunzi hao walishindwa kusoma maneno yaliyoundwa na silabi zenye muundo wa konsonanti mwambatano, maneno ya lugha ya kiingereza ambayo hayana uhusiano wa moja kwa moja kati ya umbo na matamshi yake. Pia, walionesha kutokuwa na umahiri katika kujibu maswali ya ufahamu yaliyotokana na kifungu cha maneno. Aidha, asilimia 3.52 ya wanafunzi walishindwa kusoma neno lolote katika sentensi walizopewa. Vile vile asilimia 12.12 ya wanafunzi walishindwa kujibu vipengele vyote vya maswali yaliyotokana na kifungu cha maneno walichokisoma.

Katika Stadi ya Kuandika wanafunzi wengi (89.19%) walikuwa na utendaji wa wastani hadi mzuri sana. Hata hivyo, asilimia 10.82 walikuwa na utendaji hafifu kwani walishindwa kuandika majina ya vitu katika picha, kutofautisha maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa na ndogo na pia walishindwa kunakili kifungu cha maneno na kuweka alama za uandishi. Aidha, katika umahiri wa kutumia alama za uandishi asilimia 74.6 walishindwa kutumia alama ya koma (,).

Ulinganifu uliofanyika kwa kuzingatia lugha ya kufundishia na mahali shule ilipo unaonesha kuwa, shule zinazofundisha kwa kutumia lugha ya kiingereza zilikuwa na kiwango kizuri cha utendaji ikilinganishwa na shule zinazotumia lugha ya Kiswahili kufundishia. Aidha, shule za mijini zimeonesha kuwa na kiwango kizuri cha utendaji ikilinganishwa na shule za vijijini katika stadi zote tatu.

Uchambuzi zaidi wa taarifa za shule unonesha kuwepo kwa mabadiliko chanya katika baadhi ya changamoto za ufundishaji na ujifunzaji zilizobainika katika Upimaji wa KKK 2017. Kwa mfano, changamoto ya upatikanaji wa mihtasari haikubainika kwa kuwa shule zote 66 sawa na asilimia 100 zilizofanya upimaji 2018 zilikuwa na mihtasari husika ya KKK.

Aidha, uwepo wa vifaa na miundombinu muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji kama vile vyumba vya madarasa na samani umeongezeka.

## 6.2 Mapendekezo

Kwa ujumla utendaji wa wanafunzi wa Stadi zote tatu uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2018. Ili kuongeza zaidi utendaji wa wanafunzi katika Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza:

(a) Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia (WyEST) kupitia Idara ya Udhibiti Ubora wa shule na Uongozi wa Elimu ngazi ya Mkoa, Wilaya na Shule wafuatilie ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu ili kufanyia kazi changamoto zilizobainika.

(b) Uongozi wa Elimu ngazi ya Mkoa, Wilaya na Shule kwa kushirikiana na wazazi ufuatilie mahudhurio ya wanafunzi shuleni ili wanafunzi wote walioandikishwa Darasa la Kwanza waweze Kusoma, Kuandika na Kuhesabu kwa ufasaha wafikapo Darasa la Tatu.

(c) Walimu wanaofundisha Stadi ya Kusoma watilie mkazo ufundishaji wa maneno yenye kosonanti mwambatano, maumbo tofauti na matamshi na kusoma kwa ufahamu.

(d) Walimu wanaofundisha Stadi ya Kuandika watoe mazoezi ya kutosha katika kuandika herufi, silabi na maneno, kutambua maneno yaliyoandikwa kwa herufi kubwa na ndogo na kunakili vifungu vya maneno na kuweka alama za uandishi.

(e) Walimu wanaofundisha Stadi ya Kuhesabu watoe mazoezi ya kutosha katika kukamilisha mfuatano wa namba hususani unaopungua kwa achano la mbili au tano, kujumlisha kwa kubeba, kutoa kwa kukopa, hesabu za fedha na maumbo.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
# UPIMAJI WA DARASA LA PILI

201 STADI YA KUSOMA

Muda: Dakika 15 Ijumaa, 12 Aprili 2019 asubuhi

## Maelekezo

1. Karatasi hii ina **maswali matatu (3).**
2. Mwanafunzi anatakiwa kujibu maswali **yote kwa mdomo.**
3. Kila mwanafunzi atapimwa kwa **dakika 15.**
4. Msimamizi anatakiwa kujaza taarifa za mwanafunzi katika nafasi zilizo wazi juu ya fomu maalum ya upimaji kwa **kalamu ya wino wa bluu.**
5. Mwanafunzi atakapokuwa amemaliza kusoma, msimamizi anatakiwa kujaza alama katika fomu maalum ya upimaji kwa kutumia **kalamu ya wino mwekundu.**

## Kusoma Maneno

Mwongoze mwanafunzi kusoma maneno kwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Mwoneshe mwanafunzi (kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia neno la kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari.

(ii) Mwelekeze mwanafunzi kusoma maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo.

(iii) Hakikisha mwanafunzi anatumia **sekunde tatu tu**, kusoma kila neno. Baada ya sekunde tatu mwelekeze mwanafunzi kusoma neno linalofuata.

(iv) Usomaji wa maneno utafanyika kwa **dakika tatu**, ambapo **dakika moja** itatumiwa na mwanafunzi katika usomaji na **dakika mbili** zitatumiwa na msimamizi kukokotoa alama na kujaza fomu maalum ya upimaji.

1. Mwanafunzi asome maneno yafuatayo:

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| televisheni | gita | vitamini | wiki | picha |
| kompyuta | pini | mdomo | sentensi | nyumba |
| tochi | Baiskeli | mwanafunzi | ubao | mwavuli |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| chumvi | saa | mbwa | mwezi | kikombe |
| mchele | mkono | mwanga | karoti | jogoo |

## Kusoma Sentensi

Mwongoze mwanafunzi kusoma sentensi kwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Mwoneshe mwanafunzi (kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari.

(ii) Mwelekeze mwanafunzi kusoma sentensi kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo.

(iii) Hakikisha mwanafunzi anatumia **sekunde tatu tu**, kusoma neno katika sentensi. Baada ya sekunde tatu mwelekeze mwanafunzi kusoma neno linalofuata.

(iv) Usomaji wa sentensi zote utafanyika kwa **dakika nne**, ambapo **dakika moja** itatumiwa na mwanafunzi katika usomaji na **dakika tatu** zitatumiwa na msimamizi kukokotoa alama na kujaza fomu maalum ya upimaji.

2. Mwanafunzi asome sentensi zifuatazo:

(i) Mbuzi wangu wana mikia mifupi.

(ii) Njoo hapa dada yangu mpole.

(iii) Tafadhali fungua kitabu chako vizuri.

(iv) Viatu vyangu vyote ni vyeusi.

(v) Hawa ni watoto wadogo sana.

## Kusoma Kifungu cha Maneno

Mwongoze mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Mwoneshe mwanafunzi kifungu cha maneno (kwa kugusa kwa kalamu) kuanzia sentensi ya kwanza kutoka kushoto kwenda kulia katika kila mstari na mweleze mwanafunzi kuwa akimaliza kusoma, utachukua karatasi yake na utamuuliza maswali yanayohusiana na kifungu cha maneno alichosoma.

(ii) Mwelekeze mwanafunzi kusoma kifungu cha maneno kwa sauti, umakini na haraka kadri awezavyo. Mwanafunzi atakapokuwa anasoma, fuatilia usomaji wake kwa kutumia kifungu cha

maneno kilichopo katika fomu maalum ya Upimaji.

(iii) Mwanafunzi akimaliza kusoma, chukua karatasi yake ya upimaji kisha muulize maswali yaliyopo katika **fomu maalum ya Upimaji**.

(iv) Usomaji wa kifungu cha maneno utafanyika kwa **dakika nane**, ambapo **dakika tatu** zitatumiwa na mwanafunzi katika usomaji na **dakika tano** zitatumiwa na msimamizi kukokotoa alama na kujaza fomu maalum ya Upimaji.

3. Mwanafunzi asome kifungu cha maneno kifuatacho kisha ajibu maswali atakayoulizwa na msimamizi kwa mdomo:

Furaha ana umri wa miaka nane. Anaishi Kinondoni na kaka yake mkubwa. Mara zote hutunza vitu vyake vizuri. Siku ya Jumatatu, Furaha alikwenda dukani kununua Penseli. Alikuwa na shilingi mia tano mfukoni. Alinunua penseli mbili kwa shilingi mia nne. Furaha alibaki na shilingi mia moja ambazo alizitumia kununua kifutio.

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

## Fomu Maalum ya Kujaza Alama za Mwanafunzi katika Upimaji wa Kusoma

Jina la Mwanafunzi_______________________________

Namba ya Mwanafunzi____________________________

Jina la Shule____________________________________

Wilaya_________________________________________

Mkoa__________________________________________

| KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU | | |
|---|---|---|
| **Namba ya Swali** | **Alama** | **Saini ya Mpimaji** |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| **Jumla** | | |

1. Kusoma maneno (alama $12^1/_2$)

Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi alipokosea kusoma neno na akarudia kwa usahihi, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama $00^1/_2$**)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| televisheni | gita | vitamini | Wiki | Picha |
| kompyuta | pini | mdomo | sentensi | nyumba |
| tochi | baiskeli | mwanafunzi | ubao | mwavuli |
| chumvi | saa | mbwa | mwezi | kikombe |
| mchele | mkono | mwanga | karoti | jogoo |

**Alama:** ☐

2. Kusoma sentensi (alama 25)

Weka alama ya **mkwaju (/)** kwa kila neno katika sentensi ambalo mwanafunzi **ameshindwa** kulisoma. Iwapo uliweka alama ya mkwaju mwanafunzi aliposahihisha kusoma neno alilokuwa amekosea, zungushia **(Ø)** neno hilo. (Kila neno **moja** sahihi **alama** 1)

| |
|---|
| Mbuzi wangu wana mikia mifupi. |
| Njoo hapa dada yangu mpole. |
| Tafadhali fungua kitabu chako vizuri. |
| Viatu vyangu vyote ni vyeusi. |
| Hawa ni watoto wadogo sana. |

**Alama:**

3. Kusoma kifungu cha maneno kisha kujibu maswali kwa mdomo (alama $12^1/_2$).

Sikiliza kwa makini wakati mwanafunzi anasoma kifungu cha maneno. Baada ya mwanafunzi kusoma,

chukua karatasi aliyokuwa anasoma kisha muulize maswali yaliyopo chini ya kifungu cha maneno.

Furaha ana umri wa miaka nane. Anaishi Kinondoni na kaka yake mkubwa. Mara zote hutunza vitu vyake vizuri. Siku ya Jumatatu, Furaha alikwenda dukani kununua Penseli. Alikuwa na shilingi mia tano mfukoni. Alinunua penseli mbili kwa shilingi mia nne. Furaha alibaki na shilingi mia moja ambazo alizitumia kununua kifutio.

**Maswali na Majibu**

Endapo mwanafunzi atatoa jibu sahihi kuanzia kipengele (a) hadi (c) zungushia alama 3 na kipengle (d) alama $3^1/_2$, iwapo atatoa jibu lisilo sahihi zungushia alama 0 na kisha andika jumla ya alama katika nafasi kwenye jedwali lifuatalo:

| **Na** | **Maswali na majibu** | **alama** | |
|---|---|---|---|
| (a) | Furaha ana umri wa miaka mingapi? **(nane)** | 3 | 0 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (b) | Furaha anaishi na nani? **(kaka yake mkubwa)** | 3 | 0 |
| (c) | Furaha alikwenda wapi siku ya Jumatatu? **(dukani)** | 3 | 0 |
| (d) | Furaha alitumiaje shilingi mia tano aliyokuwa nayo? **(alinunulia penseli mbili na kifutio)** | $3^1/_2$ | 0 |
| **Jumla Alama** | | | |

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

# NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL OF TANZANIA

## STANDARD TWO ASSESSMENT

**201 READING SKILLS**

Time: 15 Minutes Friday, 12th April 2019 morning

### Instructions

1. This paper has **three (3) questions**.
2. Pupils should answer **all** questions **orally**.
3. Every pupil will be assessed for **15 minutes**.
4. The invigilator is required to fill in the pupil's information on the blank spaces at the top of the Assessment form by using a **blue pen**.
5. When the pupil has finished reading, the invigilator is required to fill in the marks on the **special assessment form** by using a **red pen**

## Reading of Words

Guide the pupil to read words by considering the following:

(i) Show the pupil (by pointing with a pen) starting from the first word from left to the right in each row.

(ii) Instruct the pupil to read words loudly, carefully and as quickly as possible.

(iii) Make sure that the pupil use **only three seconds** in reading each word. After three seconds, instruct the pupil to read the next word.

(iv) Reading of words will take **three minutes,** of which **one minute** will be used by the pupil to read and **two minutes** will be used by the invigilator to calculate marks and fill in the assessment form.

1. The pupils should read the following words.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| television | guitar | vitamins | week | picture |
| computer | pin | mouth | sentence | house |
| torch | bicycle | pupil | blackboard | umbrella |
| salt | watch | dog | moon | cup |
| rice | arm | light | carrot | cock |

## Reading of Sentences

Guide the pupil to read the sentences by considering the following:

(i) Show the pupil (by pointing with a pen) starting from the first sentence from left to right in each row.

(ii) Instruct the pupil to read the sentence loudly, carefully and as quickly as possible.

(iii) Make sure that the pupil uses **only three seconds** in reading each word in the sentence. After three seconds, instruct the pupil to read the next word.

(iv) Reading of all sentences will be done for **four minutes,** in which **one minute** will be used by

the pupil to read and **three minutes** will be used by the invigilator to calculate marks and fill in the assessment form.

2. The pupil should read the following sentences:
   (i) My goats have short tails.

   (ii) Come here my calm sister.

   (iii) Please, open your book carefully.

   (iv) All my shoes are black.

   (v) These are very young children.

**Reading of a paragraph**

Guide the pupil to read the paragraph by considering the following:

(i) Show the pupil the paragraph (by pointing with a pen) starting from the first sentence from left to right in each row and instruct the pupil that when he/she has finished reading, you will take his/her paper and ask him/her questions which are related to the paragraph.

(ii) Instruct the pupil to read the paragraph loudly, carefully and as quickly as possible. When the pupil is reading, trace his/her reading by using the paragraph which is in the assessment form.

(iii) When the pupil has finished reading, take his/her assessment paper and ask him/her questions which are in the **special assessment form.**

(iv) Reading of the paragraph will take **eight minutes,** in which **three minutes** will be used by the pupil to read and **five minutes** will be used by the invigilator to calculate marks and fill in the assessment scale paper.

3. The pupil should read the following paragraph and answer the questions which will be asked by the invigilator orally:

Furaha is eight years old. She lives at Kinondoni with her elder brother. She always keeps her

things properly. On Monday, Furaha went to the shop to buy pencils. She had five hundred shillings in her pocket. She bought two pencils for four hundred shillings. Furaha remained with one hundred shillings which she used to buy an eraser.

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL OF TANZANIA

## The Special Form to Fill in Pupil's Marks for Reading Assessment

Name of the Pupil ______________________________

Pupil's Number_________________________________

Name of the School _____________________________

District ______________________________________

Region ______________________________________

| FOR ASSESSOR'S USE ONLY | | |
|---|---|---|
| **Question Number** | **Marks** | **Assessor's Signature** |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| **Total** | | |

1. Reading of words (**12$^1/_2$** marks)

Put a **slanted slash mark (/)** in each word which the pupil has **failed** to read. Circle **(Ø)** if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed. (The score for each correct word is **00$^1/_2$ mark)**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| television | guitar | vitamins | week | picture |
| computer | pin | mouth | sentence | house |
| torch | bicycle | pupil | blackboard | umbrella |
| salt | watch | dog | moon | cup |
| rice | arm | light | carrot | cock |

**Marks:**

2. Reading of the sentences (25 marks)

Put a **stroke mark (/)** in all words in a sentence which the pupil has **failed** to read. Circle **(Ø)** if the pupil re-reads correctly the word which you had slashed (The score for each correct word is **1 mark**)

My goats have short tails.

Come here my calm sister.

Please, open your book carefully.

All my shoes are black.

These are very young children.

**Marks:**

| |
|---|
| |

3. Reading of the paragraph and answering the questions orally (**$12^1/_2$** marks)

Listen carefully while the pupil is reading the paragraph. When he/she has finished reading, collect the paper which the pupil was reading and then ask him/her the questions from the paragraph.

Furaha is eight years old. She lives at Kinondoni with her elder Brother. She always keeps her things properly. On Monday, Furaha went to the shop to buy pencils. She had five hundred shillings in her pocket. She bought two pencils for four hundred shillings. Furaha remained with one hundred shillings which she used to buy an eraser.

**Questions and Answers**

If a pupil will give a correct answer, circle 3 marks for letter (a) up to (c) and **$3^1/_2$** marks for letter (d), if he/she will give an incorrect answer, circle

the 0 mark and then write the total marks in the space provided in the table.

| No. | Question and Answer | Marks | |
|---|---|---|---|
| (a) | How old is Furaha? **(Eight years)** | 3 | 0 |
| (b) | Who lives with Furaha? **(Her elder brother)** | 3 | 0 |
| (c) | Where did Furaha go on Monday? **(To the shop)** | 3 | 0 |
| (d) | How did Furaha spend her five hundred shilings? **(She used it to buy two pencils and an eraser)** | $3^{1}/_{2}$ | 0 |
| **Total** | | | |

Kiambatisho Na. 5: Karatasi ya Upimaji Stadi ya Kuandika

**Jina la Mwanafunzi__________________**

**Namba ya Mwanafunzi ______________**

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
# UPIMAJI WA DARASA LA PILI
# 202 STADI YA KUANDIKA



**Muda: Dakika 40 Alhamisi, 11 Aprili 2019 asubuhi**



## Maelekezo

1. Karatasi hii ina maswali **matatu** (3).
2. Jibu maswali **yote**.
3. Andika **majibu yako yote** kwa kutumia penseli.
4. Andika **jina** lako na **namba** yako katika kila ukurasa.

| KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU | | |
|---|---|---|
| Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| **Jumla** | | |

1. **Tazama kwa makini picha zifuatazo kisha andika majina yake** katika nafasi zilizo wazi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) | <br>______________ | (b) | <br>______________ |
| (c) | <br>______________ | (d) | <br>______________ |

| | | | |
|---|---|---|---|
| *(e)* | <br>____________________<br>_ | *(f)* | <br>________________________ |
| *(g)* | <br>__________________ | *(h)* | <br>_____________________ |
| *(i)* | <br>___________________ | *(j)* | <br>________________________ |

2. **Pigia mstari** maneno yaliyoandikwa kwa **herufi kubwa**.

(a) MKATE, chungwa, mlima, KIJIKO

(b) BLUU, kijani, NYEKUNDU, manjano

(c) SAA, mkuki, CHAKI, karatasi

(d) Paka, SIMBA, pundamilia, NYANI

(e) SHATI, sketi, GAUNI, suruali

3. **Nakili** kifungu cha maneno kifuatacho na kisha weka alama za uandishi yaani: **nukta (.), mkato (,), alama ya kushangaa (!),** na **alama ya kuuliza (?)** mahali panapostahili.

Jamani eeh__ Basi la kwenda nyumbani kwetu limetuacha__ Sasa je__ tutaondoka na usafiri wa basi gani__

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

Pupil's Name____________________

Pupil's Number __________________

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL OF TANZANIA
# STANDARD TWO ASSESSMENT

202 WRITING SKILLS



Time: 40 Minutes Thursday, 11th April 2019 morning


## Instructions

1. This paper has **three (3) questions**.
2. Answer **all** questions.
3. Write **all your answers** in pencil.
4. Write your **name** and **number** on every page.

| FOR ASSESSOR'S USE ONLY | | |
|---|---|---|
| Question Number | Marks | Assessor's Signature |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| Total | | |

1. **Study** the pictures below **carefully** and then **write** their names in the spaces provided.

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) |  ____________________ | (b) |  ____________________ |
| (c) |  ____________________ | (d) |  ____________________ |
| (e) |  ____________________ | (f) |  ____________________ |

| | | | |
|---|---|---|---|
| (g) |  ________________ | (h) |  ________________ |
| (i) |  ________________ | (j) |  ________________ |

2. **Underline** the words which are written in **capital letters**.

(i) BREAD, orange, mountain, SPOON

(ii) BLUE, green, RED, yellow

(iii) WATCH, spear, CHALK, paper

(iv) Cat, LION, zebra, MONKEY

(v) SHIRT, skirt, DRESS, trousers

3. **Copy** the following paragraph in the space given and then put the punctuation marks: **full stop (.), comma (,) exclamation mark (!)** and **question mark (?)** where necessary.

My goodness __ The bus has already left __ So __ which bus are we going to travel by __

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

________________________________________________

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
# UPIMAJI WA DARASA LA PILI

## 203 STADI YA KUHESABU

Muda: Saa 1 Alhamisi, 11 Aprili 2019 asubuhi

## Maelekezo

1. Karatasi hii ina maswali **ishirini (20)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Andika majibu yote kwa **penseli**.
4. Andika **namba** na **jina** lako katika kila ukurasa.

| KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji | Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji | Namba ya Swali | Alama | Saini ya Mpimaji | Namba ya Swali | Alama | S ai n |
| 1. | | | 7. | | | 13. | | | 19. | | |
| 2. | | | 8. | | | 14. | | | 20. | | |
| 3. | | | 9. | | | 15. | | | | | |
| 4. | | | 10. | | | 16. | | | | | |
| 5. | | | 11. | | | 17. | | | | | |
| 6. | | | 12. | | | 18. | | | | | |

Andika namba inayokosekana katika nafasi iliyoachwa wazi.

1. 4, 5, ___, 7, 8, 9.

2. 15, ___, 13, 12, 11.

3. 44, 46, ___, 50, 52.

4. 70, 80, 90, ___.

5. 25, 30, ___, 40, 45.

Tafuta Majibu:

6. 1 + 7 = ________

7. 12 + 5 = ________

8. 28 + 6 = ________

9. 47 + 16 = ________

10. Shilingi 400 + shilingi 50 = ________________

11. 8 - 5 = ________

12. 19 - 4 = ________

13. 25 - 7 = ________

14. 67 - 18 = ________

15. Shilingi 700 - shilingi 550 = ________

16. Mary ana machungwa 240 na kaka yake ana machungwa 342. Je, jumla wana machungwa mangapi?

________________________________________

________________________________________

________________________________________

_______________________________________

17. Sara alikuwa na pipi 450. Alimgawia rafiki yake pipi 220. Je, alibakiwa na pipi ngapi?

________________________________________

________________________________________

________________________________________

_______________________________________

18. Darasa la pili lina wasichana 70 na wavulana 90. Je, darasa hilo lina wanafunzi wangapi?

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

_______________________________________

19. Juma alinunua kalamu kwa shilingi 150 na daftari kwa shilingi 500. Je, alilipa shilingi ngapi?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

____________________________

20. Musa alipewa shilingi 600 na baba yake. Alitumia shilingi 250. Je, alibakiwa na shilingi ngapi?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

_____________________________________________

Jina la Mwanafunzi_________________

Namba ya Mwanafunzi ______________

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL OF TANZANIA
## STANDARD TWO ASSESSMENT
## 203 ARITHMETIC SKILLS

**Time: 1 Hour Thursday, 11th April 2019 morning**

### Instructions

1. This paper has **twenty (20)** questions.
2. Answer all questions.
3. Write your answers in pencil.
4. Write your name and your number on each page.

| FOR ASSESSOR'S USE ONLY | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Question Number | Score | Assessor's Initials | Question Number | Score | Assessor's Initials | Question Number | Score | Assessor's Initials | Question Number | Score | Assessor's |
| 7. | | | 7. | | | 13. | | | 19. | | |
| 8. | | | 8. | | | 14. | | | 20. | | |
| 9. | | | 9. | | | 15. | | | | | |
| 10. | | | 10. | | | 16. | | | | | |
| 11. | | | 11. | | | 17. | | | | | |
| 12. | | | 12. | | | 18. | | | | | |

Write the missing number:

1. 4, 5, ___, 7, 8, 9.

2. 15, ___, 13, 12, 11.

3. 44, 46, ___, 50, 52.

4. 70, 80, 90, ___.

5. 25, 30, ___, 40, 45.

Work out the answers:

6. 1 + 7 = ________

7. 12 + 5 = ________

8. 28 + 6 = ________

9. 47 + 16 = ________

10. 400 shillings + 50 shillings = ________________

11. 8 - 5 = ________

12. 19 - 4 = ________

13. 25 - 7 = ________

14. 67 - 18 = ________

15. 700 shillings - 550 shillings = ________

16. Mary has 240 oranges and her brother has 342 oranges. How many oranges do they have altogether?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

17. Sara had 450 sweets. She gave her friend 220 sweets. How many sweets was she left with?

______________________________________________

______________________________________________

18. A standard two class has 70 girls and 90 boys. How many pupils are in the class?

______________________________________________

______________________________________________

__________________________________________________________________________________________________________________________

19. Juma bought a pen for 150 shillings and an exercise book for 500 shillings. How much did he pay?

20. Musa was given 600 shillings by his father. He spent 250 shillings. How much money was he left with?

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA STADI YA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU**

**DODOSO LA MWALIMU MKUU WA SHULE**

**Jina:**__________________________________________

**Shule Unayoongoza:**______________________________

**1. Taarifa za shule kwa ujumla**

*Tafadhali jaza taarifa kuhusu wanafunzi na walimu wa KKK katika shule yako kwa kuandika katika visanduku ulivyopewa.*

(i) Kuna wanafunzi wangapi waliodahiliwa katika darasa la I na la II waliopo shuleni kwa sasa? ☐

(ii) Walimu wangapi wanafundisha stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu darasa la I na la II katika shule yako? ☐

(iii) Kati ya walimu wanaofundisha stadi za KKK, Walimu wangapi wana mafunzo maalumu ya kufundisha stadi hizo? ☐

(iv) Je shule ina mikondo mingapi ya wanafunzi wa darasa la I? ☐

(v) Mikondo ya wanafunzi wa darasa la I uliyoitaja katika (iv) hapo juu ina wanafunzi wangapi kila mmoja (jaza wastani kama idadi hailingani) ☐

(vi) Je shule ina mikondo mingapi wa wanafunzi wa darasa la II? ☐

(vii) Mikondo ya wanafunzi wa darasa la II uliyoitaja katika (iv) hapo juu ina wanafunzi wangapi kila mmoja (jaza wastani kama idadi hailingani) ☐

Je shule ina Muhtasari wa Kufundishia stadi za KKK kwa darasa la Kwanza na la Pili? Ndiyo ☐ Hapana ☐

## 2. Taarifa kuhusu Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia.

*Tafadhali jaza maoni yako kuhusu uwepo wa vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia kwa kuzungushia namba ya uchaguzi unaolingana na maoni yako kuhusu vifaa hivyo hapo shuleni kwako.*

| SN | Swali | Hafifu (2) | Chini ya Wastani (2) | Wastani (3) | Mzuri (4) | Mzuri Sana (5) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (i) | Upatikanaji wa Vitabu vya kiada vya kufundisha stadi za Kuhesabu unaweza kuelezewa kuwa ni: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| (ii) | Upatikanaji wa vitabu vya ziada vya mazoezi ya stadi ya kuhesabu unaweza kuelezewka kuwa ni: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| (iii) | Uwepo wa Vifaa vya kufundishia stadi ya kuhesabu (kama vile vihesabio na vifaa vingine) unaweza kuelezewa kuwa ni; | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| (iv) | Uwepo wa Vifaa vya kufundishia stadi ya Kuandika (kama vile vibao na vifaa vingine) unaweza kuelezewa kuwa ni; | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| (v) | Je uwepo wa vitabu vya kiada vya kufundishia stadi ya kusoma unaweza kuelezewaje? | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| (vi) | Je unaweza kuelezeaje upatikanaji wa viafaa vinavyolenga kuendeleza stadi ya kusoma kama vile vitabu vya hadithi fupifupi kwa watoto wadogo? | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

## 3. Taarifa kuhusu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji

*Tafadhali jibu maswali kuhusu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzungushia namba inayolingana na maoni yako kuhusu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK katika shule yako.*

| SN | Swali | Hafifu (2) | Chini ya Wastani (2) | Wastani (3) | Mzuri (4) | Mzuri Sana (5) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| (i) | Uwepo wa madawati, viti na meza za kukalia watoto na walimu shuleni kwako wakati wa kujifunza unaweza kuelezewa kuwa ni: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| (ii) | Ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi wa darasa la I na la II waliopo shuleni kwa sasa, hali ya uwepo wa vyumba vya madarasa inaweza kuelezewa kuwa ni: | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
| (iii) | Je mazingira ya upatikanaji wa chumba maalumu au makataba ambapo watoto na walimu wanaweza kuazima vitabu ili kuwawezesha wanafunzi kujifunza zaidi stadi za KKK hata baada ya muda wa shule yakoje? | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

## 4. Taarifa nyinginezo

Je ni jambo gani ambalo halikuulizwa kwenye dodoso hili kuhusu mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji ambalo ungependa Baraza la Mitihani lifahamu? (Toa maelezo mafupi)

**5.** **Changamoto zinazojitokeza wakati wa ujifunzaji wa wanafunzi wa stadi za KKK kuwa mgumu**

*Tafadhali jibu maswali kuhusu changamoto zinazojitokeza ambazo zinafanya ujifunzaji wa wanafunzi wa stadi za KKK kuwa mgumu kwa kuzungushia namba ya changamoto inayojitokeza zaidi. (unaweza kuzungushia changamoto zaidi ya moja)*

.

(i) Umbali wa wanafunzi wengi kutoka shule ilipo

(ii) Wanafunzi kukosa masomo mara kwa mara kutokana na mahudhurio yasiyoridhisha

(iii) Uhaba wa walimu ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi

(iv) Kupokea wanafunzi wanaohamia ambao stadi zao za KKK haziridhishi.

(v) Uhaba wa vitendea kazi kama vile vitabu ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi.

(vi) Changamoto nyinginezo (Zitaje)

**Kiambatisho Na. 10: Dodoso la Msimamizi**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**UPIMAJI WA STADI YA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU 2019**

**DODOSO LA MWALIMU (MSIMAMIZI)**

**Jina:**______________________________ **Mkoa** ______________________

**Halmashauri** _____________________ **Shule :** _____________________

**Mkondo Uliosimamia:** __________ **Namba ya Simu:**________________

1. Je, umesimamia idadi ya wanafunzi wangapi katika stadi ya :
   (i) Kuandika ☐
   (ii) Kuhesabu ☐
   (iii) Kusoma ☐

2. Je wakati wa kusimamia vifaa vyote vilivyohitajika katika kufanya upimaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu vilitosheleza?

   Ndiyo ☐ Hapana ☐

   (a) Kama jibu ni hapana taja aina ya vifaa ambavyo havikutosheleza.

   ______________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   __________________________________________

   (b) Eleza hatua zilizochukuliwa kutatua upungufu huo.

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ____________________________________________________________

3. Je, kuna wanafunzi walioshindwa kufanya upimaji? Kama wapo waorodheshe majina yao na sababu za kushindwa kufanya upimaji.

| Na | Jina | Sababu za Kushindwa Kufanya Upimaji |
|---|---|---|
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |

4. Umewahi kupokea kitabu chenye taarifa ya uchambuzi wa upimaji wa KKK wa mwaka 2017 na kukitumia?.

Ndiyo ☐ Hapana ☐

5. (a) Unafikiri vitabu hivyo vina tija katika kuborehsha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK?

Ndiyo ☐ Hapana ☐

(b) Toa maelezo mafupi kwa jibu lako hapo juu.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

***Asante kwa ushirikiano***